

TAZAMA, ALIYE MKUU

KULIKO SULEMANI YUPO HAPA

 Asante, Ndugu. Mungu akubariki.

² Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kurudi hapa usiku wa leo, na kuwa katika ibada ya Bwana. Na bila shaka tulifurahia jana usiku, kutoa maoni tu, ujumbe, mchezo mdogo wa kuigiza. Vema, kamwe hamkuufurahia zaidi ya nilivyofurahia, kujaribu kuwakariria, kama nionavyo, jinsi Bwana alivyolifanya, ama, walivyolifanya katika Biblia. Basi, usiku wa leo, ni majaliwa makubwa sana kurudi hapa, usiku wa leo, na kuwaona ninyi nyote mmerudi tena, hilo ni jambo zuri sana.

³ Ninataka kusema, ya kwamba mara nydingi katika mikutano ambapo ninii, inaeleweka vibaya, huduma ya namna hii, lakini hakika inaonekana inaeleweka vizuri hapa, na hiyo inaonyesha ya kwamba mmekuwa na mafundisho mazuri, ninathamini hilo.

⁴ Na sasa, daima angalieni yale anayowaambieni, mnaona. Sina wakati, usiku wa leo, wa kulielezea, jinsi... angalieni tu yale anayosema, kwa sababu si mimi, sijui. Mnaona, ni ninii tu, kama vile ningejaribu kusema, ninii tu, ni karama, kama vile gia unajiingizia tu. Wala hujui, bali wewe ndiwe unayefanya jambo hilo, wewe ndiwe, si mimi.

⁵ Na wale wanaosafiri, na katika u....barabarani, na kadhalika, na nyumbani, maono yanayokuja kule si kama yalivyo jukwaani. Yale ya jukwaani, unayafanya mwenyewe, unaona, hujui, bali unayafanya, ni imani yako inayoyafanya. Nayo yale ya nyumbani ndiyo ambayo Mungu anafanya, na *haya* ndiyo unayofanya wewe.

⁶ Kama vile ningewaelezea kifupi tu, wakati yule mwanamke alipoligusa vazi la Bwana Yesu, mwanamke aligeuka, ama, Yeye aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Ndipo akaangalia kote, nao, mtume Petro kwa namna fulani akamkemea kwa kutoa tamshi kama hilo, Naye akasema alitambua ya kwamba alidhoofika, nguvu zilitoka, kutoka kwa maskini mwanamke mmoja. Naye akaangalia kote katika hilo kusanyiko mpaka akampata, akamwambia, kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Imani yake, imani yake ilikuwa imefanya hivyo, mnaona, imani yake.

⁷ Vema, sasa, vipi kuhusu wakati alipomfufua Lazaro? Jinsi hilo lilivyokuwa ni jambo kubwa zaidi kumwita mtu arudi baada ya kufa siku nne! Hakuna neno lililosemwa kuhusu Yeye kudhoofika hapo. Mnaona? Huyo alikuwa ni Mungu akifanya hilo. Sasa, katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin,

nawaambia, Mwana hawesi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda kwanza.” Mnaona? Mnaona, lilikuwa ni ono. Sio, “lile ninalomsikia Baba analisema,” bali, “lile nimwonalo Baba analitenda.” Mnaona?

⁸ Sasa, Bwana alikuwa amemwambia... Tunajua Maandiko hayatatanishi, wala hayajipangi, Yenyewe ni ya kweli, kwa hiyo basi Yeye hakufanya neno mpaka Baba alipomwonyesha kwanza kwa ono jambo la kutenda, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawesi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile. Baba anatenda kazi, natenda kazi vile vile.” Kwa maneno mengine, ni kufanya tu mchezo wa kuigiza, yale Mungu aliywambia afanye.

⁹ Sasa, hapana shaka Mungu alimwambia, basi, amwache Lazaro na aende zake, kwa sababu alikuwa yuaenda kufa, baada ya siku *kadha* wangetuma mtu, bali asiende, kwa sababu familia hiyo nzuri ilikuwa ikiagizia aitwe, Nayé akazidi kusonga mbele.

¹⁰ Basi hatimaye, Lazaro, alipokufa kwenye saa hiyo na kadhalika, Yesu alijua hilo, ndipo akageuka na kusema, “Lazaro amelala.” Bila shaka, hawakuelewa hilo, walidhani alikuwa akipumzika, ndipo akawaambia katika lugha yao wenyewe, “Amekufa. Na kwa ajili yenu nina furaha sikuwapo, lakini ninaenda kumwamsha.” Mnaona?

¹¹ Sasa, mwangalieni kaburini, “Baba, ninakushukuru kwamba Wewe tayari umenisikia Mimi, lakini nasema haya kwa ajili ya wale wanaosimama hapa.” Mnaona? Hakuna kitu kilichosemwa kuhusu Yeye kudhoofika, hiyo ilikuwa ni Mungu akitumia karama Yake, akitumia Mwanawe jambo la kufanya. Lakini wakati yule mwanamke alipomgusa, hiyo ilikuwa ni mwanamke akitumia karama ya Mungu kwa ajili ya imani aliyokuwa nayo ndani yake. Mnaona? Hiyo ndiyo tofauti. Mnaona, ni imani yako, si yangu, yako. Wewe ndiwe unayefanya jambo hilo, ni imani yako.

¹² Ni muda mfupi sana wa kukaa, kundi zuri sana la watu, hata kwa namna fulani ninachukia kuondoka, ingawa nimechoka. Lakini sina budi kuninii... Sasa, najua, usiku wa leo, wana ibada ya—ya ubatizo, na kadhalika, hapa kanisani. Ndugu Ned Iverson, rafiki yangu na ndugu, attachukua ibada sasa na kuendelea kwa muda, nami bila shaka ningempendekeza, ningependekeza kwamba mje, mumsikie.

¹³ Na kwa hiyo basi, usiku wa leo, baada ya ibada, hatuna budi kuondoka mapema vya kutosha kwa ajili ya jambo hilo, nami sina budi kwenda kwenye moteli yangu, na kijiandaa, na kuondoka saa kadhaa kabla hakujapambazuka, asubuhi, na kuendesha maili mia saba, ili nipate kuanzia nyumbani kesho yake asubuhi, saa tisa ama kumi nyumbani usiku, ili juma lijalo niwe, huko Cow Palace Los Angeles. Sina budi kwenda kwa gari pamoa na familia yangu. Sina siku zingine, bali kusafiri tu, siku

moja na mbili kati ya hiyo mikutano, hadi Septemba hii ijayo, nalo ni jukumu kubwa sana, kwa hiyo niombeeni.

¹⁴ Nami si mkubwa sana, na kama ningalikuwa mkubwa kama mchungaji wenu, hapa, ninaamini ningeweza tu kwenda mchana na usiku; siwaambii mumtumie mchana na usiku. Lakini—lakini maskini Ndugu Ned alisema, leo, nilipokuwa nikizungumza naye pamoja na mchungaji, kasema, “Laiti ningaliweza kukuhamishia baadhi ya nguvu zangu.”

Nikawazia, “Vema, hilo lingekuwa jema,” maana yeye ni mkubwa sana na mwenye nguvu, nami daima nilikuwa mdogo.

¹⁵ Nilipokuwa nikifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma, ningepanda vipandio, ndi—ndipo opereta aliye juu, mtambo wa kubadilishia, Binti Ehalt, akasema, “Billy, sikuzote ninaweza kujua wakati una—ninii, unapokuja,” kasema, “wewe ndiwe mtu mdogo sana anayefanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma na mwenye kelele kuliko wote.”

Nikasema, “Vema, Edith, inanibidi kupiga kelele nyingi sana kuwafanya watu wajue niko humu.” Kwa hiyo . . .

¹⁶ Sasa, ninaamini ndugu wote wametambulishwa, nafikiri, kote mstarini. Na maskini ndugu mmoja niliyemwacha kwenye mkutano huo mwengine, na huyo ni maskini mvulana huyo wa Kimethodisti ambaye alikuwa Mmethodisti shupavu sana kutoka kwenye seminari, pia—pia tuna ndugu ambaye ni mashuhuri sana huko—huko Asbury, Wilmore, Kentucky, naye mvulana huyu na familia yake walikuwa na kupokeea ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakihubiri Injili Yote, na huyo ni Ndugu Collins, Willard Collins. Uko wapi, Willard? Willard Collins, mahali fulani huko nyuma kabisa. Je, ungetaka tu kusema neno kutoka hapo? Ama, njoo huku juu, ningetaka mtu fulani amwone Mmethodisti aliye na Roho Mtakatifu, mbali na Ndugu Neville hapa, njoo hapa, na useme tu neno kwetu.

¹⁷ Nami nadhani, Ndugu Junior Jackson, ametambulishwa, sivyo, Ndugu Jackson? Mmethodisti mwengine, shupavu kabisa, na aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹⁸ Ndugu Collins, nimemjua kwa miaka kadhaa, Mkristo mzuri, wa thamani, mtu halisi wa Mungu. Yeye na mke wa—wake na familia wote wako chini ya utaratibu wa Mungu wa Biblia.

Ndugu Collins, Mungu akubariki.

[Ndugu Collins anasema maneno machache—Mh.]

Asante, Ndugu Collins, Bwana akubariki. Hilo ni zuri sana.

¹⁹ Sasa, enyi Wamethodisti hapa, hatumaanishi kwamba wewe si Mkristo. Unaona? Lakini mnajua kanisa la Kipentekoste ni nini? Kanisa la Kimethodisti lililoendelea mbele. Unaona?

²⁰ Naye Jack Shuler, wengi wenu mnajua, ninyi Wamethodisti wazuri, Jack aliniambia, wakati mmoja nilipokuja

Phoenix, nami nilikuwa nikienda Madison Square Garden, alikuwa nje, ukumbi wa shule, nami nikampigia simu, nikasema, “Jack, sikujua ulikuwa hapa.”

Akasema, “Ndugu Branham, sikujua ulikuwa unakuja,” naye akasema, “Ningekuondokea.”

²¹ Nikasema, “Nisingekuja kama ningejua ulikuwa hapa.” Nikasema, “Vema, Ndugu Jack,” nikasema, “karibu watu wote wanaohudhuria mikutano yangu ni Wapentekoste.”

Akasema, “Vema, unalo kundi langu.”

Nikasema, “Nilifikiri wewe ni Mmethodisti.”

Akasema, “Vema, hivi hujui Methodisti ni nini?”

Nami nikasema, “La.”

Kasema, “M—M—Mmethodisti, au, Mpentekoste ni Mmethodisti wa kiothodoksi.”

Nanyi nyote mlajua, labda wengi wenu mnamjua Jack, na Mzee Bob, na hao wengine, walikuwa Wakristo halisi.

²² Nilikuwa katika chuo cha—cha Kilutheri, Bethania, ambako walinikemea, loo, jamani, wakinichimbua tu, yeye ndiye, aliyenita mpiga ramli mkubwa, ndipo kwa namna fulani Bwana akamfuatilia kidogo kwa ajili ya hilo, mwajua, na kwa hiyo akanipigia simu kuniomba msamaha. Tukashuka kwenye orofa ya chini ambako waliandaa mlo mkuu wa kutwa, naye akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, ninataka tu kukuuliza maswali machache. Kwanza, samahani nilisema yale niliyosema katika barua hiyo.”

Nikasema, “Hiyo ni sawa, hata sikuwazia tena juu yake.”

Akasema, “Nataka uniambie, ni nini kamwe...? Je, sisi Walutheri tuko kwenye shindano?”

Nikasema, “Hakika.”

Akasema, “Tu—tu—tuna nini?”

²³ Nikasema, “Mna Roho wa Mungu.” Kisha nikasema, “Mnajua...” Wao, kwa wanafunzi ambaio wasingewenza kulipia masomo yao, kwa hiyo, walikuwa na kama ekari elfu moja za mahindi kule, kwa hiyo wakafanya kazi tu. Kwa hiyo wao... Akasema... Nikasema, “Mtummoja wakati mmoja alipanda zao la mahindi, naye akatoka, ndipo kesho yake asubuhi kulikuwa na majani mawili madogo yaliyojitokeza, akasema, ‘Bwana asifiwe kwa ajili ya zao langu la mahindi!’”

Nikasema, “Sasa, Ndugu Hegre, alikuwa na zao la mahindi?”

Akasema, “Vema, bado.”

Nikasema, “Kwa uwezekano alikuwa nalo, sivyo?”

Akasema, “Naam.”

²⁴ Nikasema, "Huyo alikuwa ni ninyi Walutheri." Nikasema, "Muda si muda, hayo majani mawili madogo yakakua, na baada ya kitambo kidogo yakatoa kishada, hicho kilikuwa ni Methodisti. Wakaangalia chini na kusema, 'Huna faida tena, wewe ni jani tu, mimi ni kishada.'

²⁵ "Ndipo baada ya kitambo kidogo baadhi ya chavua zikaanguka kutoka kule zikaangukia jani tena, nazo zikazaa suke la mahindi, kama ile punje asili iliyoingia ardhini." Nami nikasema, "Hiyo ilikuwa ni ya Kipentekoste," nikasema, "lakini mnaona, ile punje asili." Nikasema, "Tuna kuvu nyingi sana kwenye suke, lakini hata hivyo kuna punje mle pia, mwajua. Lakini wao . . ." Nikasema . . . Nami nikasema, "Sasa, kanisa la Kipentekoste ni Lutheri iliyoendelea mbele." Akaliona.

²⁶ Akasema, "Vema, Ndugu Branham, tu—tulisoma habari zake," kisha kasema, "tulishuka huko," pia kasema, "tumeona Wapentekoste wakiruka, na kutikisika, na kupiga viti teke." Kasema, "Wa—wana nini?"

Nikasema, "Roho Mtakatifu."

Akasema, "Vema, ni kitu gani kinachowafanya wafanye hivyo?"

Nikasema, "Inawabidi kutoa mvuke. Mnaona?" Na—nami nikasema . . .

Akasema, "Unaamini hilo?"

²⁷ Nikasema, "Hakika, lakini, unaona, jambo ni kwamba, kanisa la Kipentekoste, nda . . . ambapo, kosa pekee ninalowapata nalo, ni kwamba wao huutoa kwa filimbi, badala ya kuuweka kwenye gurudumu na kuyafanya yafingirike." Mtu anaposema neno dhidi yako, kama neema hiyo ya Mungu ikisimama pale kuwapenda haidhuru, ndiyo hiyo, acha huo mvuke ufanye kazi hapo, mnaona, na—na kutoka kwenda nje mtaani, na kuwaingiza wengine, na kadhalika, acha—acha—acha mvuke ufanye kazi papo hapo.

²⁸ Ninapenda kuusikia ukilipuka pia, mwajua, lakini ngoja mpaka utakapofika kwenye kivuko, ndipo tunaweza kuulipua, mnaona. Hebu na tuyafanye yafingirike wakati tunapokimbia kwenye uwanja wa mbio upesi sana. Na kwa hiyo wao . . .

²⁹ Nimealikwa tena kwa neema na mchungaji wenu, na labda, Bwana akipenda msimu huu wa kupukutika, nitakaporudi, ninaweza kuja siku zingine chache usiku, msimu huu wa kupukutika.

³⁰ Naye Ndugu Bigby, nilimwomba alete makala hiyo tena aliyoandika. Mbona, kila kitu kimesemwa kunihusu mimi, mwajua, Nimeitwa kila kitu kuanzia Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili hata pepo aliye duni mno. Na, lakini nafikiri usemi wake ulikuwa wa hakiki, aliutamka kutoka moyoni mwake, haikuwa ni kujipendekeza, ilikuwa tu ni kile alichowazia,

na mimi—mimi bila shaka nathamini hilo. Ninaninii tu... Ni karibu makala bora sana niliyowahi kupata kunihusu mimi. Nami nilikuwa na kadhaa pale, lakini kila mmoja aliyeingia, “Naweza kuchukua hili, Ndugu Branham?” Na muda is muda, yameniishia, mnaona, kwa hiyo nilimwomba kama angejaribu kuniletea mengine ya hayo, maana kuna vitabu vingine vinavyokuja, navyo vita—vitaninii... Nataka hiyo makala mle, pamoa na jina lake.

³¹ Na, jambo lingine, nafikiri walitoa vitabu, huko nyuma. Nafikiri hiyo ni kweli, sivyo? Ndugu Wood na hao wengine, na kanda, na kadhalika, kama vile, huko nyuma, mnapotoka nje.

³² Na sasa, tunaninii... Ninanawasihi nyote mniombee. Mimi huwa naenda kuwaombea watu, na halafu, vema, mimi—mimi ndimi ninayehitaji maombi, ninyi, labda ni vigumu kwenu kuelewa hilo, lakini hiyo ni kweli. Ni... Ninayahitaji vibaya sana labda kuliko ninyi nyote, na labda si kwa njia ya maradhi, bali kwa njia ya yale ambayo sina budi kukabiliana nayo siku baada ya siku.

³³ Na kila siku, kuna watu wanaoketi papa hapa sasa, wakinangalia moja kwa moja, ambao nilikuwa nao kwenye mahojiano asubuhi ya leo, na kadhalika, na wanaajua jinsi, inahitaji tu Roho wa Mungu kuingia mle ndani, na kupata himzo nyufa na kona maishani.

³⁴ *Hili ni Neno, tunaamini hilo, na hilo ni Neno, bali Mungu aliweka Kanisani mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti, na mambo hayo yote yanakamilisha.* Na, sasa, walimu, na wachungaji, na wainjilisti, hao ndio wanaoleta Neno, nao manabii wanapaswa kutafuta-tafuta kwenye maskini kona himzo ndogo kwa ajili ya watu binafsi, mnaona, na kutabiri mambo yajayo, na kadhalika.

³⁵ Mitume kwa kweli ni wamishenari. Ninaamini, sasa, elimu yangu ni haba sana, lakini, nafikiri neno *mitume* linamaanisha “mtu aliyetumwa.” Hiyo ni kweli? Hivi *mmishenari*, si ni kitu kile kile? “Mtu aliyetumwa.” Kwa hiyo jinsi walivyopata kutamani kuitwa *wamishenari*, badala ya *mitume*, sijui mimi, lakini lolote lile ni sawa, kama Bwana... mradi tu Bwana alimtuma, hilo ni sawa.

³⁶ Sasa, sitachukua muda wenu mwingi, kwa ajili ya ibada ya ubatizo inayokuja moja kwa moja, ninataka kusoma Maandiko fulani, nami natumaini haitanichukua muda mrefu sana.

³⁷ Nilisema jana usiku, “Nipeni dakika thelathini,” nami nilipokuwa nikishuka barabarani, baada ya kujaribu kujirudia kutokana na kubembea kutoka kwenye zile milki mle ndani, mwanangu alisema, “Hizo zilikuwa dakika ishirini kamili, Baba.” Kasema—kasema, “Yapata tu saa moja na arobaini na tano.”

³⁸ Nikaangalia, “Loo, sikuwa huko muda mrefu hivyo, nisingeweza kuwa,” ndipo nikaangalia hapa kwenye saa yangu ya mkono, nikasema, “Naam.” [Ndugu fulani anasema, “Amina. Chukua muda wako, chukua muda wako.”—Mh.] Lakini unajua, ni jambo fulani kuhusu... Asante. Ni jambo ambalo... [Ndugu mwengine anasema, “Amina. Wewe endelea mbele, usiku kucha.”] Wananipenda. Wa—wa—wananipenda, nami nawapenda pia. Niliweza kukutana na baadhi ya hao ndugu huko nje na kushika mkono huo wa maskini moyo halisi, mzuri wa kusini ukidunda chini pale, kweli napenda hilo.

³⁹ Lakini mnajua, wakati mwengine, kila mhudumu anajua wakati Roho Mtakatifu anaonekana tu kuninii, kila neno unalosema linazama tu ndani, si ni hisia nzuri sana? Unachukia tu kumaliza, sivyo? Naam. Na hata hivyo, unajua wewe ni fidhuli na unakatiza mikutano, lakini ni vigumu kwako kumaliza.

⁴⁰ Inanikumbusha, nina wasichana wawili wadogo nyumbani. Nao ni wasichana wazuri sana sasa, wakubwa kidogo, mmoja wao ana umri wa miaka kumi na sita, na huyo mwengine ana kumi na miwili, mmoja wao ni Rebekah, na huyo mwengine ni Sarah, na Sarah ni jamaa mdogo.

⁴¹ Vema, miaka michache iliyopita, basi, nilikuwa nikija kutoka mkutanoni. Na wote wawili ni wasichana wa baba, loo, jamani, mnajua jinsi... Naye maskini mvulana huyo mdogo, maskini, humm, nena kuhusu... alisema atakuwa mhubiri, nikasema, “Mpenzi, una mengi ya kufanya marekebisho, endapo utakuwa.” Na kwa hiyo, Joseph.

⁴² Na kwa hiyo, hao wasichana walikuwa bado ni wadogo sana, nao walikuwa wakikesha mpaka yapata usiku wa manane nipate kuingia. Nami nilikuwa nimechoka, na nilikuwa nikiendesha gari, loo, siku mbili ama tatu, nikiingia kutoka California. Basi nilipofika nyumbani, bila shaka wasichana hao wadogo walikuwa wameshikwa na usingizi na tayari wameenda kulala, naye Mama alikuwa akingojea. Kwa hiyo nikajilaza chini kujaribu kulala, wala kamwe nisingeweza kufanya hivyo, na, mwajua, kutetemeka, na wasiwasi, na kadhalika kutoka kwenye huo mkutano, athari zake, nafsi, na kutambua wajibu huo wote wa kushikilia hao walionunuliwa kwa Damu ya Kristo mbele yako. Si jambo rahisi tu. Ndugu hapa wanajua ni kitu gani, jinsi wewe...

⁴³ Nafikiri kila mhudumu anapaswa kukaa peke yake muda mrefu kabla ya kuingia mimbarani, apate kutoka katika upya wa Roho Mtakatifu, anao hao walionunuliwa. Mnaona, mara nyangi nimewazia kile ningefanya na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu, na sasa hapa mbele zetu, tunao wale walionunuliwa kwa Damu Yake, Yeye alitoa Damu Yake kwa ajili yako, nasi tunalishughulikia kusanyiko hilo. Loo, jamani, afadhali tuwe na hakika kabisa, na tuwe na kicho tu tuwezavyo kuwa.

⁴⁴ Kwa hiyo nilikuwa na wasiwasi sana, kama sote tujuavyo jinsi ilivyo, nami nisingeweza kulala, kwa hiyo nilikuwa, mke wangu alingojea muda mrefu, kwa hiyo alikuwa amelala, nikaamka nikaenda nikaketi kitini, huko nje sebuleni. Yapata mapambazuko nilikuwa nimeketi pale, nikiwazia juu ya huo mkutano, na kushangaa tena baadhi ya hayo maono yalikuwa nini, na kadhalika, na mara nikasikia vitu vikianguka kule chini kwenye chumba cha msichana, moja kwa moja kupitia ukumbi mdogo kule kwenye nyumba ya mchungaji.

⁴⁵ Ndipo nikaangalia, Becky, alikuwa ameamka, upesi akawazia, "Haya ni mapambazuko, hapana shaka Baba yuko nyumbani." Basi wakati aliporuka juu, alimwamsha Sarah, dada yake mdogo. Naye Becky kwa namna fulani ni mwembamba, na ana miguu mirefu, na—na—na kwa hiyo akaja mbio chumbani, naye Sarah, maskini jamaa mfupi. Na kidogo niliwalinganisha, katika kuwazia jambo hilo, na kanisa, mwajua, limekuwako muda mrefu hapa, mwajua, nalo lina historia nyingi sana nyuma yake, na—na hilo lingine kwa namna fulani ni kundi dogo, fupi, la Kipentekoste, mwajua, wao, kwa namna fulani, hawajakaa muda mrefu sana. Kwa hiyo wao....

⁴⁶ Ndipo Becky akaja mbio sana, naye akatagaa pajani mwangu, naye akasema, akanikumbatia shingoni, akaanza kunikumbatia, nawe unajua jinsi moyo wako unavyojisikia. Vema, maskini Sarah, alikuwa amevaa, sijui kama watoto wenu hufanya hivyo au la, wangu hupochezana, mtumba, kwa hiyo alikuwa amevaa pajama za Becky, nayo miguu ilikuwa tu kama miguu ya sungura, mwajua, mirefu kupita kiasi, ndipo jamaa mdogo alikuwa akijikwaa, akianguka, na akipitia nyumbani, hatimaye akafanikiwa.

⁴⁷ Na yapata tu wakati alipofika pale, Becky akaangalia kote, akasema, "Sarah, dada yangu, nataka kukwambia jambo fulani, nilikuwa hapa kwanza." Mnaona? Kisha kasema, "Ninaye Baba wote, wala hakuna kitu kilichosalia kwako."

⁴⁸ Kwa hiyo maskini Sarah, maskini mdomo wake mdogo ukainama chini, macho yake madogo ya hudhurungi kidogo yamelowa maji. Nikachomoa mguu wangu mwingine nje, nikamwashiria. Akakimbia tu na kuurukia moja kwa moja, kama vile angefanya kwa farasi wa matandiko, naye kidogo alikuwa anapepesuka, mwajua, yeYe, karibu kuanguka. Hakuwa amekaa huku muda mrefu sana, miguu yake haikuwa mirefu kama ya Becky, angeweza kufika chini kabisa sakafuni, mwajua.

⁴⁹ Na—na kwa hiyo, Sara alikuwa akipepesuka, nami nikamkumbatia kwa mikono yote miwili kumshika. Akalaza kichwa chake juu ya kifua changu kidogo, moja kwa moja upesi akayafungua hayo macho madogo meusi, na kumwangalia Rebekah, kasema, "Rebekah, dada yangu, nataka kukwambia jambo fulani." Mnaona? "Huenda ikawa ni kweli kwamba

unaye Baba wote, lakini nataka ujue Baba ana mimi wote.” Kwa hiyo...

⁵⁰ Mwajua, anapotufungia sisi sote ndani Yake, hatujali tena, sivyo? Kila kitu hufifia tu kabisa. Na hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya, na hivyo ndivyo sote tunavyotaka kufanya, acha tu Yeye achukue yote tuliyio nayo, wakati wetu wote, hisia zetu zote, na tumtolee tu Yeye, hiyo ni kweli.

⁵¹ Sasa hebu tusome sehemu ya Neno la thamani sasa, kabla hatujazungumza juu Yake tena, kwa muda kidogo tu. Na hebu tufungue katika Biblia sasa, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, kwenu ninyi mnaotaka kuandika hili somo, na hebu tuanzie kwenye mlango wa 12 na kifungu cha 38, kuendelea pamoja na kifungu cha 42:

Hapo palikuwapo na baadhi ya waandishi na Mafarisayo, wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta...ishara; wala hakitapewa...ishara, ila ishara ya nabii Yona:

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawakumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁵² Na kama ningיטה neno dogo ambalo ningetaka kutoa kutoka hapo, *Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa*.

⁵³ Alikuwa akiwakemea hao Mafarisayo kwa kutokuamini kwa—kwao, walikuwa na Biblia za magombo kote katika nyakati, ambapo manabii wote waliokuwa wamenena habari za kuja Kwake. Kote tangu Musa alipoandika Mwanzo, alinena juu ya kuja kwa Masihi.

⁵⁴ Musa alimwelezea, kile Yeye angekuwa hasa, jinsi ambavyo ninii... Naye Isaya akaeleza jinsi angezaliwa, jinsi kuzaliwa Kwake kungekuwa kwa bikira. Naye Musa alinena ya kwamba Yeye angekuwa ni Nabii tu kama yeye. Na mambo haya yote yalikuwa yamesemwa juu ya Bwana wetu.

⁵⁵ Na hata hivyo, m—mfumo wa siku hizo ulikuwa ndio kwanza ufanye, uondoke kwenye Neno, nao walikuwa na

kile walichokuwa wakiishia, mapokeo yao ya wazee. Nami natumaini makanisa yetu hayatakuwa hivyo kamwe, kuachana na kuliamini Neno la Mungu, kuyaendea mapokeo ya wazee. Ndipo tunaunda mafundisho ya sharti, kisha tunaweka mambo katika—katika, Fundisho letu ambalo kweli haliko katika Biblia. Nami natumaini daima tutadumu katika Injili yote, na kuhubiri Injili yote wakati wote, sisi sote. Hivyo—hivyo ndivyo ninavyofikiri ya kwamba Mungu alikusudia, kwetu kuhubiri tu hilo jambo lote.

⁵⁶ Na sasa, kama nilivyosema mara nyingi, huenda nisiwe na imani ya kufanya kila ahadi itimie, lakini hakika nisingemzua mtu ambaye alikuwa na imani ya kutosha kufanya hivyo. Mara nyingi nimesema ningetaka kuwa na imani ya kutosha kama Henoko alivyokuwa nayo, hata isinibidi kufa wakati wangu utakapofika, nifanye tu matembezi ya alasiri, nipande niende Nyumbani pamoja Naye, bali kama sina imani hiyo, hakika ninatumaini nitapata kumwona mtu aliye nayo. Nami nitatumaini ya kwamba siku moja sote tutakuwa na imani hiyo, ili kwamba wakati Yeye atakapokuja tunawenza tu kutembea na kwenda Nyumbani pamoja Naye.

⁵⁷ Sasa, Yesu alikuwa kabisa, kama tulivyoona jana usiku katika ule mchezo mdogo wa kuigiza, kwamba Yeye angetekeleza kikamilifu, na kutenda vile vile hasa Maandiko yalivyosema angetenda. Na wengi wa hao walikuwa wameamini kwa sababu, hata kama vile yule mwanamke kisimani, mara huyo Roho na tendo alipomulika moyoni mwake, alijua upesi ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Kulikuwako na... Masihi, wakati alipokuja, alikuwa afanye kazi ya namna hiyo, kwa hiyo yeye akasema, “Hapana shaka Wewe ni nabii.”

⁵⁸ Sasa, mnaona, wakati mwengine tunapuuza kitu ambacho ni kizuri sana, kwa sababu hakina m—mng’aro tunaofikiri kinapaswa kuwa nao. Sitaki kuondoka kwenye somo langu, lakini hapa miaka kadhaa iliyopita nilikuwa nikisoma ambapo kwamba—kwamba kulikuwa na mtu aliye kuwa amefanya u—uhalifu, naye alikuwa, alikuwa amewekwa gerezani, na kuhukumiwa, na kupatikana na hatia ya jambo alilokuwa amefanya alipokuwa kazini, basi ilikuwa ni wakati wa Abraham Lincoln, nao walikuwa wakitaka kumpiga risasi huyo mtu kwenye machweo ya juu asubuhi *fulani*.

⁵⁹ Rafiki mwema aliyempenda, basi akamtetea, wala asingeweza kupata jibu, kwa hiyo akaenda kwenye chanzo kikuu zaidi alichoweza, akaenda kwa Bw. Lincoln. Walisema ya kwamba Bw. Lincoln alikuwa akishuka kwenye gari, naye akaanguka mbele yake na kusema, “Bw. Lincoln, Mheshimiwa...” akaelezea kisa hicho. Naye akasema, “Yeye ni mtu mzuri.”

⁶⁰ Nafikiri alikuwa ametoroka wakati wa jambo fulani, vita,

ama hakutii agizo aliloagizwa ama chochote kile, na kwa hiyo, ama... Naye akasema, "Alikuwa tu na wasiwasi, alitoka kwenye nyumba nzuri." Kisha kasema, "Alikuwa tu na wasiwasi na kufadhaika. Bw. Lincoln, hakukusudia kufanya hivyo. Na kesho kutwa asubuhi watampiga risasi, atakufa kwa kikosi cha kulenga shabaha, kesho kutwa asubuhi."

⁶¹ Kasema, "Bw. Lincoln, wewe ni Mkristo." Kasema, "Wewe... Sahihi yako moja ingeyasamehe maisha ya mtu huyo." Kisha kasema, "Hakukusudia kufanya hivyo, nina hakika." Kasema, "Ninamwombea kama rafiki."

Bw. Lincoln akachukua kipande cha karatasi, na kuandika tu juu yake, kasema, "Amesamehewa, na Abraham Lincoln."

Akaipeleka kwa huyo mtu gerezani, asingeipokea. Akasema, "Wewe iwasilishe."

⁶² Asingeipokea, akasema, "La. Kama ingekuwa ni ya Bw. Lincoln, ingepaswa kutiwa muhuri kwa muhuri wa Marekani," na kadhalika, na yote namna hiyo, akasema jinsi ambavyo hiyo rangi ingebidi kuwa juu yake. Basi kwa sababu aliukataa, aliuawa. Kwa sababu aliukataa huo... Hiyo hapo ninii ya Bw. Lincoln..., ama—ama, jina, sahihi, bali aliukataa.

⁶³ Ndipo basi ilifanyiwa kesi mahakamani, kwa sababu hilo hapo jina lake, kasema ya kwamba—ya kwamba alimsamehe mtu huyo, kisha mtu huyo akapigwa risasi, kwa hiyo wakati ilipofanyiwa kesi katika mahakama ya shirikisho, huu hapa uamuji wa mahakama ya shirikisho: "Msamaha si msamaha, isipokuwa ukubaliwe kama msamaha." Kwa hiyo hivyo ndivyo Neno la Mungu lilitivo. Ni Neno la Mungu kwa wale wote watakaolikubali kama Neno la Mungu, la sivyo, vema basi, silo.

⁶⁴ Kwa hiyo tunaamini Neno, na hiyo ndiyo sababu tunaitazamia ile ishara ya kuonekana Kwake. Hatutaki kukosea katika jambo hilo, nasi tunataka kuninii... hatutaki kuchukua mawazo ya mtu fulani kulihusu, tunataka kulisoma moja kwa moja kutoka kwenye Neno.

⁶⁵ Kwa hiyo Yesu alikuwa amefanya moja kwa moja na kikamilifu, kila ishara aliypaswa kufanya. Sasa, tunajua pia, kabla hatujaondoka kwenye, sehemu hii ya somo, kwamba Wayahudi wanatafuta ishara, mnaona, Wayunani, hekima. Naye Paulo akasema, "Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa." Sasa, Wayahudi, wakitafuta ishara kwa sababu wao—wao waliweka ishara juu ya theolojia yao. Na likuwa ni jambo zuri. Kama...

Huenda ukasema, "Sasa, kidogo hilo linasikika la kigeni, Ndugu Branham."

⁶⁶ Vema, Yesu alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Mnaona? Kama Yeye hakulithibitisha Ne—Neno la Mungu, basi msimwamini. Lakini Yeye alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, basi liaminini Neno."

⁶⁷ Sasa, tunaona katika Biblia, kama mtabiri, ama mwotaji, aliota ndoto nao hawakuwa na hakika juu yake, waliwapeleka hekaluni na kuwaweka mbele ya Urimu na Thumimu. Nanyi mnaona, iwapo Urimu na Thumimu haikujibu... Sasa, utafiti wa karibu sana ninaoweza kupata juu ya jambo hilo, kwamba Urimu na Thumimu ilikuwa nini, ilikuwa ni hii naivera ya Haruni. Niliichukua hivi majuzi kwenye moja ya mikutano mikuu huko kwenye uwanja wa Baptisti ya Marekani, huko Green Lake, Wisconsin, ambako Wafanyabiashara wa Full Gospel walikuwa na mkutano, nao walikuwa na mfano wa hayo mawe kule, yote.

⁶⁸ Sasa, basi wakamchukua mwotaji, ama mtabiri, haidhuru ilionekana ni zuri jinsi gani, kama nuru hizo za ajabu, kama upinde wa mvua, zikimetameta kwenye Urimu na Thumimu hiyo, basi ndoto hiyo haikukubaliwa, wala unabii. Ilijaribiwa na Urimu na Thumimu. Kwa hiyo, mnaona, ya kimbunguni ndiyo iliyothibitisha ukweli daima.

⁶⁹ Sasa, nawazia jambo lile lile siku hizi. Tunaposikia mengi sana kwamba siku za miujiza zimepita, nanyi Wapentekoste na watu wa full Gospel mmeenda kombo, nafikiri ni kwa sababu hawaelewii. Baada ya hiyo Urimu na Thumimu ya wakati huo wa makuhani, ama, wakati huo kwisha, na wakati wa Haruni, wakati wa makuhani wa Walawi, tuna Urimu na Thumimu nyingine, na Hiyo ni Biblia ya Mungu. Mnaona? Na kama ishara zetu na maajabu yakitokea, Neno la Mungu linayaakisi, basi tunaweza kusema, “Amina” kwake. Ni Mungu akithibitisha yale hasa aliyohahidi kufanya.

⁷⁰ Aliahidi angemwaga Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, kwa hiyo ni uakisi tu, ni—ni *hii* Urimu na Thumimu ikijiakisi Yenyewe ndani ya watu. Nina hakika hilo si gumu kueleweka mionganii mwa watu wa namna hii. Ni Urimu na Thumimu *hapa*, Biblia, ikiakisi ahadi za Mungu.

⁷¹ Naye Yesu alikuwa ameakisi ofisi Yake kama Masihi, nao walikuwa hawajaamini. Na katika milango ifuatayo tunaelewa ya kwamba wao, ama, m—mlango ule ule, uliotangulia huu, walikuwa wameziona kazi Zake, nao walikuwa wamemwita, “Beelzebuli.” Beelzebuli ni ibilisi, kama ninii, walikuwa wamemwona akifanya mambo hayo, nao walidhani Yeye alikuwa ni mpiga ramli, ama mchawi, ama kitu fulani.

⁷² Naye akawaambia, “Sasa, mnanena dhidi ya Hili, nami nitawasamehe, lakini Roho Mtakatifu ajapo,” labda kufanya jambo lile lile, ndivyo Yeye alivyomaanisha, “kunena dhidi ya Huyo hakutasamehewa kamwe,” mnaona, kwa sababu... “katika—katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.

⁷³ Sasa, sasa, Mungu katika nyakati zote, daima alikuwa na karama katika Kanisa Lake. Daima amewathibitisha watu Wake. Popote mnapomwona Mungu aliye hai, mnaona ishara za

Mungu aliye hai. Sasa, huyo hapo Moabu juu ya kilima, naye alikuwa akitoa sadaka, alikuwa na madhabahu saba, Balaamu alikuwa nayo, pia alikuwa na mafahali saba, alikuwa na kondoo dume saba, yule fahali, dhabihu safi, kondoo dume wakinena juu ya Yule mwenye haki ajaye.

⁷⁴ Kimsingi, alikuwa wa kimsingi tu kama—kama Musa alivyokuwa huko chini kambini pamoja na Israeli, lakin tofauti pekee ilikuwa kwamba Mungu alikuwa akimthibitisha Musa kwa Mwamba uliopigwa, na nyoka wa shaba, na Nguzo ya Moto, na sauti ya . . . kambi, kambini, ya Mfalme mle ndani. Naye Mungu alikuwa akithibitisha jambo hilo kule chini, hiyo ndiyo tofauti. Hiyo inaonyesha . . .

⁷⁵ Sasa, kama tukizungumza kimsingi, sasa, Kaini alikuwa wa kimsingi tu kama Habil alivyokuwa. Wavulana wote wawili walikuwa wakitaka kupata kibali kwa Mungu. Kaini alilet dhabihu, Kaini akajenga madhabahu, Kaini akaabudu, mnyofu tu kama Habil alivyokuwa, bali Habil, kwa ufunuo wa kiroho, ambapo Kanisa limejengwa juu yake, juu ya ufunuo wa kiroho wa mapenzi na Neno la Mungu, alitoa dhabihu ambayo Mungu aliifurahia. Na sasa, ninaamini hiyo ndiyo siku tunayoishi sasa, pia.

⁷⁶ Sasa, Mungu sikuzote alikuwa na ishara. Yesu, hapa, alikuwa akizungumza juu ya, akiikemea miji hiyo na kusema, “Loo, ewe Kapernaumu,” na mingine mbalimbali, “kama zile ishara, kama zile kazi kuu zilizofanywa kwako ambazo, ama, zingalifanywa Sodoma, zilizofanywa kwako, ingebakia hata leo, nawe umeinuliwa hata Mbinguni, lakini utashushwa hata kuzimu.” Angewezaje . . . Akiikemea miji ambayo haikuupokea huo Ujumbe.

⁷⁷ Basi angalieni Ujumbe siku hizi, jinsi umeenea ulimwenguni, wamishenari. Loo, ninaamini itakuwa rahisi zaidi kwa Sodoma na Gomora kuliko itakavyokuwa kwa hao watu, na ile miji siku hizi inayoikataa Injili, wakati Mungu akiwa na Urimu na Thumimim Yake anaakisi ishara na maajabu Yake ya siku za mwisho mionganoni mwa watu Wake. Angalia tu kile ambacho kimefanywa katika miaka michache iliyopita: Kote ulimwenguni mioto ya uamsho inaendelea kwa ishara kuu na maajabu, na mambo ya kimiujiza. Hakuwezi kuwa na kitu kinachowenza kufuata hiyo ila Hukumu, baada ya kukataliwa.

⁷⁸ Sasa, Yesu alikuwa akizungumza hapa juu ya baadhi ya watu katika siku ambazo Mungu alikuwa ameonyesha ishara. Mmoja aliyenena habari zake alikuwa ni Yona, naye Yona alitumwa kwenda Ninawi. Nami daima nilimhurumia Yona, kwa sababu watu wengi, nafikiri, walikosa kumwelewa Yona. Sasa, walisema Yona alikuwa amerudi nyuma, alikuwa *hiki, kile, na kinginecho*, nami nimesema vivyo hivyo, lakini hebu na tumchunguze tu Yona kwa dakika moja.

⁷⁹ Siamini kwamba alikuwa amerudi nyuma, kwa sababu alikuwa ni nabii wa Mungu, naye alionekana alikuwa akitoka nje ya Mapenzi ya Mungu, lakini hii hadithi ndogo ninayotaka kuwasimulia hivi punde, ninaamini mtaona ya kwamba Mungu aliyafanya yote yatendeke vizuri kabisa.

⁸⁰ Mnajua, nyayo za wenyе haki zinaongozwa na Bwana. Hiyo inatupa sisi wahudumu wakati...nafasi wakati mwingine ya kupumua tunapofikiri tumechukua hatua mbaya. Lakini wakati mwingine Mungu anatembea tu pamoja nasi, tunafikiri ni makosa, lakini labda ni Mungu akitenda kazi.

⁸¹ Sasa, Ninawi ulikuwa ni mji mkubwa kuliko huu, naam, karibu ukubwa wa St. Louis, nao ulikuwa ni mji wa makafiri, pia ulikuwa ni mji mashuhuri, wa kibiashara, na mji mkuu wa pwani ya bahari. Moja ya biashara zao kuu kule ilikuwa ni kuvua samaki. Nao walikuwa ni waabudu sanamu, nazo dhambi zao zilikuwa ni kubwa sana hata Mungu asingeweza kuvumilia jambo hilo tena.

⁸² Kumbukeni, hapakuwapo na dhabihu madhabahuni kwa ajili yao wakati huo, kama ilivyo kwa ulimwengu siku hizi, kwa hiyo Mungu asingeweza kuvumilia dhambi hiyo ya kutisha, kwa hiyo akamwambia nabii Wake ashuke aende Ninawi, sote tunaifahamu hiyo hadithi sisi tusomao Biblia, na kusema, "Piga kelele juu ya mji huo."

⁸³ Ndipo huyo nabii, alipotelemka hata pwani ya hiyo bahari, badala ya kwenda Ninawi, alichukua merikebu iliyokuwa ikisafiri kwenda Tarshishi. Sasa, daima tumefikiri hiyo ilikuwa njia ya mkato, ama, kukwepa wajibu, lakini nitajaribu kumtetea mhubiri huyo usiku wa leo, nami nitasema ya kwamba ninaamini alikuwa ni nabii, naye alikuwa kabisa katika mapenzi ya Mungu. Ninaamini alifuata mwongozo wa Roho, ninaamini aliongozwa kuititia njia hiyo. Hakulielewa, baada ya Mungu kumwagizia mahali pamoja, na hapa akajikuta akipitia njia nyininge.

⁸⁴ Akashuka kwenye gubeti la hiyo merikebu, ama, chini sehemu ya mbele, akalala, ndipo tufani kubwa ikatokea. Vema, tunajua ya kwamba wote walipaza sauti ya kwamba wata—watazama, na kulikuwa na kasoro. Ndipo Yona akaja, na kukiria ya kwamba huenda ikawa ni kosa lake, akasema afungwe miguu yake na mikono yake, akatupwe baharini, kwa sababu haikuwa haki kwa wote kuangamia kwa sababu yake.

⁸⁵ Sasa, Mungu alikuwa na samaki mkubwa, tunamwita nyangumi, wa kummeza, naye huyo samaki alikuwa akila majini katika tufani hiyo. Wengi wenu mnaona jinsi samaki watakavyojitokeza, hasa sana katika tufani, wapate kula, kwa sababu kuna kingi, ba—bahari ina uamsho, mwajua, inarukaruka, ikiwa na wakati mzuri. Hapo ndipo ni...Huo ni uamsho.

⁸⁶ Ninakumbuka wakati niliposimama kando ya ufuo wa bahari kwa mara ya kwanza, haikuwa bahari, ilikuwa ni

Ziwa Michigan, Nilikuwa tu mhubiri mvulana, nikapanda kwenda kumsikiliza Paul Rader akihubiri kwenye Maonyesho ya Ulimwengu, yapata mwaka wa 1933, naamini ndio huo, na wakati ulipokuwa huko Chicago. Nami nilipata nafasi yangu ya kwanza kutembea na kuangalia ule mkusanyiko mkubwa wa maji, mkubwa kuliko Mto Ohio, nao ulikuwa tu ukiruka, na kuendelea, mwajua, na ilikuwa ni mapema majira ya kuchipua, ibada ya mapambazuko ya Pasaka tulikuwa kule. Nami nikaona hayo mawimbi makubwa meupe yakiingia, mwajua, na kugonga u—ukingo, na kufingirika, Nikawaza, “Hiyo ni . . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuimba, “Mafuriko ya furaha juu ya nafsi yangu kama mawimbi ya bahari yanavyofingirika.”

⁸⁷ Nikawazia, “Yanafingirika ndani, lakini huo sio mwisho wa wimbi, linarudi likafingirike tena, kufingirika ndani.” Nikawaza, “Vema, inaruka-ruka kwa nini? Yote ni nini . . .?” Ndipo kitu Fulani kilionekana tu kuniambia, “Ina uamsho, hivyo tu.”

⁸⁸ Vema, nikawaza, “Unajua nini? Hakuna hata chembe moja, hakuna hata tone moja la maji mahali hapo sasa, katika ziwa hilo, kuliko yangalikuwako kama ilikuwa tulivu kabisa.” Hakuna maji zaidi, hata kidogo. Uliwahi kuwazia hilo? Ila yana uamsho tu, mnaona, kuruka tu, na kupiga mayowe, na kupaza sauti, kuwa na uamsho.

Nikawaza, “Vema, kuna faida gani kuwa na uamsho?”

⁸⁹ Kulikuwa na upopo ulioshuka, upopo ukienda kasi, mwajua, kama tunavyoamini, na kuanza kulichochea. Linachochewa kwa sababu gani? Ndipo ikatokea niliona ya kwamba takataka zote zilizokuwa huko baharini, zimezolewa ufukoni. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu ya uamsho, kuosha takataka zote, mnaona, kuutoa ulimwengu wote nje, na kuufingirishia tu ufukoni.

⁹⁰ Sasa, wakati sisi . . . Natumaini makanisa yetu ya Kipentekoste hayahitaji mmoja wa huo sasa, mnaona. Tunao tu wa kufurahia, mwajua, ingawaje makanisa yetu kweli hayauhitaji. Kwa hiyo, *ahem*, tuna—tunao uamsho kwa vyovoyote vile. Kwa hiyo basi, ina—inaruka-ruka tu na kucheza-cheza huko nje kwenye mawimbi.

⁹¹ Kwa hiyo basi, wakati merikebu hii ikiruka-ruka, na samaki wakila, na muda si muda mwajua, nyangumi mkubwa akaja na kummeza Yona. Nami nilikuwa nikizungumza na mtu fulani kuhusu hilo hapa miaka michache iliyopita, walipomleta nyangumi huko Louisville kwa mkokoteni, gofu lake tu, ndipo mtu huyu alikuwa, akatoa tamshi juu yake.

⁹² Akasema, “Sasa, ninii, mwajua, mmesikia ile methali katika Biblia kuhusu nyangumi akimmeza Yona.” Kasema, “Nawatakeni ninyi nyote mwone ya kwamba, asingeweza kufanya hivyo. Ingekuwa ni ninii yake,” loo, mahali umio upo *hapa*, kasema, “hiyo nyangumi asingeweza kumeza

zaidi ya ninii, kama chu-chungwa, ama balungi, mahali linapotelemkia.”

⁹³ Nami nilikuwa nimesimama pale, kama tu mvulana, nikisikiliza. Nanyi mwajua, ilitokea nikawazia (Mliona? Nilisoma hayo baadaye.), nikasikiliza, nami nikawazia, “Hakika Biblia isingedanganya kuhusu hilo.” Nami nikawazia, “Isingeweza na ibaki Biblia. Wala hiyo si methali, ninaamini hiyo ni kweli.”

⁹⁴ Lakini mliona? Huyu alikuwa ni nyangumi maalum, Mungu alimwandaa huyu, huyu alikuwa amejengwa maalum kwa ajili ya tukio hilo. Mnajua, Mungu anaweza kufanya hivyo. Naam, anaweza. Yeye alijitolea Mwenyewe dhabihu huko juu, wakati mmoja, mlimani, katika Mwanzo 22. Yehova-Yire angeweza kujipatia nyangumi. Hivi hamwamini hilo? Kwa hiyo akamchukua mmoja mkubwa kutosha kummeza nabii huyu.

⁹⁵ Ndipo aliposhuka chini, na baada ya kula, yejote anajua unapomlisha samaki wako wa dhahabu, vema, unaona anashuka moja kwa moja hadi chini, anaweka maskini pezi zake chini, na kupumzika kwa sababu tumbo limejaa. Vema, huyo hapo chini akipumzika. Naye maskini nyangumi huyu, labda, akammeza Yona, kisha akashuka chini ya baharini, labda urefu wa mita nyingi, naye alikuwa anapumzika, na tumbo lilikuwa limejaa.

⁹⁶ Halafu basi, lakini mwajua, Yona kule chini katika tumbo la nyangumi huyu, huku mwani wa baharini umezungushiwa shingoni mwake, naye alikuwa katika hali mbaya. Basi akalala kichalichali, naye alikuwa katika matapiko ya nyangumi, naye akaanza kuangalia *huku*.

⁹⁷ Mnajua, watu huzungumza kuhusu, “Vema, Ndugu Branham, niliombewa jana usiku, lakini mkono wangu haujapata nafuu.” Hu-huitazamii ile ahadi, unaangalia dalili zako. Unaona?

⁹⁸ “Vema, ni-nilikuwa mgonjwa jana usiku nilipoombewa, sijapata nafuu asubuhi ya leo. Niombee tena.” Hilo ni sawa, bali kama ulilikubali mara ya kwanza, hakuna haja ya kuomba tena, kwa sababu tayari umetatuliwa, unaona, ni wako. Unaona? La. Nawe u-unaangalia dalili, inategemea kile unachoangalia. Unaona?

⁹⁹ Kwa hiyo alikuwa akiangalia dalili chini, anaangalia, vipi kama angaliziangalia huko chini? Vema, kama angaliangalia upande *huu* ilikuwa ni tumbo la nyangumi, akiangalia *huko* ilikuwani tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia ilikuwa ni tumbo la nyangumi, naye alikuwa chini ya bahari huku amefungwa mikono na miguu nyuma yake chini ya bahari, kwenye bahari yenye dhoruba, sasa, chini ya bahari. Sasa, nena kuhusu kisa cha dalili, kweli alikuwa nacho kule chini chini ya ile bahari katika tumbo la nyangumi huyu.

¹⁰⁰ Na—naye huyo hapo, mikono yake imefungwa, miguu yake imefungwa, amelala pamoja na mwani wa baharini, na kile samaki alichokuwa amekula kabla ya huu aliozungushiwa, huku amelala chini chini ya bahari. Lakini unajua nini? Asingeangalia tumbo hilo la nyangumi. Mnajua yale aliyosema? Yalikuwa ni ubatili wa uongo, kamwe hayakuwa ya kweli. Alitaka kuangalia kitu kingine. Akasema, “Mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu.”

¹⁰¹ Sasa, Yona alijua ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu hilo, kwamba aliomba na kusema, “Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, na watazame mahali hapa patakatifu na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Naye alikuwa na matumaini katika ombi hilo. Basi mnajua kile Mungu alichofanya? Sijui kama aliweka tangi la oksijeni mle ndani, ama alichofanya, bali alimdumisha hai kwa siku tatu mchana na usiku.

¹⁰² Sasa, kama Yona angeweza kuamani, chini ya hali hizo, maombi ambayo mtu fulani aliomba, mtu wa kawaida ambaye baadaye alirudi nyuma, naye Mungu akaiheshimu imani hiyo, inatupasa kufanya nini, usiku wa leo? Si kuangalia he—hekalu lililofanywa kwa mikono, bali Utukufuni, wala si mtu aliyerudi nyuma, bali Mwana wa Mungu aliyeketi pale na ninii Yake—pamoja na mavazi Yake yaliyojaa Damu apate kutuombea tunapokiri. Jinsi ambavyo hatupaswi kuangalia dalili zetu, bali kuangalia ahadi ya Mungu! Naam, bwana.

¹⁰³ “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Hivyo tu. Yeye ni Kuhani Mkuu anayeketi mkono wa kuume wa ukuu Wake Juu kutuombea tunapokiri, kile ambacho tumeamini na kukiri. Na lolote alilotufanyia, tunaweza kulikiri, na kuliamini, na Yeye yuko hapo kulitekeleza mbele za Uwepo wa Mungu. Jinsi tunavyopaswa kufurahi, wala tusiangalie dalili zozote, tuangalie yale Mungu aliyoahidi. Hiyo ndiyo ahadi.

¹⁰⁴ Sasa, tunaona hiyo ni ajabu, siku tatu mchana na usiku maskini nyangumi huyo alizunguka tu na kuzunguka majini mahali fulani huko nje, naye Yona alikuwa hai. Sasa, tunaambwa ya kwamba watu hao walipata riziki yao kwa kuvua, jinsi walivyopatia riziki yao ilikuwa ni kuvua samaki. Kwa hiyo labda wavuvi wote wako huko nje...Na mmoja wa miungu wao alikuwa ni mungu nyangumi.

¹⁰⁵ Kwa hiyo wote wako huko nje wakivua samaki baharini, na mara, huyo mungu wao akatokea, akakimbia moja kwa moja ufukoni, na kuuchomoza ulimi wake, ndipo nabii akaja akitembea moja kwa moja kutoka kinywani mwa mungu wao. Wangewezaje kujizuia kuamini? Mnaona? Hakika. Si ajabu waliwalishwa wanyama wao nguo za magunia, kwa kuwa mu—mungu wa bahari alikuwa amemtema nabii, naye akawaambia

watubu. Sasa, mnaona, Yona hakuwa nje ya mapenzi ya Mungu, alikuwa moja moja katika mapenzi ya Mungu.

¹⁰⁶ Naye Yesu alisema ya kwamba kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara. Mliona jambo hilo? Nao wataipokea, Yeye aliahidi ya kwamba wangeipokea ishara yao, akasema, "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika moyo wa nchi."

¹⁰⁷ Sasa, hiki ni kizazi kiovu na cha zinaa, tunajua hilo. Basi ni ishara gani waliyokuwa waipokee? Ishara ya ufufuo. Yesu hajafa, bali amefufuka tena, Naye yuko mionganoni mwetu.

¹⁰⁸ Tena, miji mikubwa ya kibiashara ilijojitolea kwa—kwa adui, kwa ibilisi, na kuoa, kuolewa, na uzinzi, na upotovu, na uchafu wa kila namna ulioko duniani siku hizi; na Wakristo wasioamini, mfano wa utauwa, wakaidi, wenye kujivuna, wakati wa elimu, nabii alinena habari zake. Roho Mtakatifu alisema dhahiri kwamba katika siku za mwisho utakuja wakati wa elimu, watu wangekuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kiburi, wenye kukufuru, wasiotii, wasiojizuia, na wasiowapenda walio wema.

¹⁰⁹ Unasema, "Hao ni wakomunisti, Ndugu Branham." La, bwana, hao ni washiriki wa kanisa wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake, hao nao... Kwa hiyo, tunapata ishara ya Yona, kwa kuwa Yesu Kristo yuko pamoja na watu Wake usiku wa leo, akitenda na kufanya jambo lile lile alilofanya kabla hajasulubiwa, na kufufuka tena, na anaishi pamoja nasi. Hu—huelewi huyo ni nani unayeketi pamoja naye huko nje, huyo ni mwana na binti wa Mungu. Labda ni jambo zuri hatulielewi, jinsi tunavyolielewa.

¹¹⁰ Loo, mbona, tumekusanyika katika ulimwengu wa Roho, tukiangalia Urimu na Thumimu Yake ya siku hizi za mwisho ikiakisi Uwepo Wake kwa kuwa yuko tayari kuja, Yeye anajitokeza katika umbo la Roho Mtakatifu kulichonga Kanisa Lake kuliweka tayari lipate kupokelewa. Amina. Tuna furaha sana kujua.

¹¹¹ Kwa hiyo sidhani ya kwamba Yona alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Nami naamini kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara. Sasa, na hao... Mungu kamwe hakukataa, bali daima Yeye huwapa ishara.

¹¹² Sasa, tunaona ya kwamba tunashuka kwa mtu mwingine, ambaye alikuwa ni Sulemani. Sasa, wasomaji wote wa Biblia wanajua ya kwamba siku za Sulemani zilikuwa ni wakati wa heri na furaha kuu wa Israeli. Kama... Walifanikiwa zaidi chini ya Sulemani, kwa sababu hapakuwapo na vita vyovyote, nao wakajenga hekalu, nao ulikuwa ni wakati mkuu, mzuri sana kwa Israeli. Na sababu, wakati Sulemani, mwana wa Daudi, alipochukua kitie cha enzi, vema, kamwe hakuomba kwamba

Mungu a—ampe *mengi*, bali hekima tu ya kujua jinsi ya kutawala na—na kuwaweka watu pamoja. Vema, sasa, Mungu alifanya kazi pamoja naye, Naye akampa karama ya upambanuzi. Kweli, hakika alifanya hivyo. Naye angeweza kupambanua mema na mabaya, na kadhalika, na habari zikaenea kila mahali, kote ulimwenguni, za ninii hii kuu . . .

¹¹³ Mnajua, kama Mungu katika wakati wowote, anapowaona watu, Naye anawapa karama, na, ama ishara . . . Nayo karama sikuzote hutoa ishara. Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa akiwakemea, kwa sababu Yeye alikuwa ni Karama ya Mungu, nayo ishara ya Karama ya Mungu ilikuwa ikithibitishwa. Yeye alisema, “Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini hizo kazi, kwa kuwa zinanena habari Zangu,” mnaona.

¹¹⁴ Na sasa, si lingekuwa jambo zuri usiku wa leo kama Marekani yote iliamini Karama ya Mungu kwa ajili ya siku hizi za mwisho, Roho Mtakatifu? Hakika, ni Karama ya Mungu. Sasa, wazia tu, kama waliikataa ishara hiyo na karama hiyo, ilikuwaje? Hi—hilo taifa liliingia katika machafuko. Kama waliikubali karama hiyo, basi hilo taifa lilikuwa na wakati wa heri na furaha kuu. Sasa, ndivyo ilivyuo usiku wa leo.

¹¹⁵ Wazieni, kama kila Mmarekani, usiku wa leo, anayekiri kuwa Mkristo na kumwamini Yesu Kristo angekubali na kuamini Karama ambayo Mungu ametutumia katika siku hizi za mwisho, Roho Mtakatifu. Mbona, mwajua nini? Wangeweza kumwondoa kila polisi kwenye kikosi. Wangeweza tu kuyateketiza mageреза, tusingeyahitaji tena. La, la. Kusingekuwako na ofisi tena za sheria na kadhalika, tusingezihitaji. Mbona, ule Utawala wa Miaka Elfu ungeanza. Hakika.

¹¹⁶ Lakini wanafanya nini? Wanaikataa Karama ya Mungu, isitoshe, bali, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wanaitania, na kuidhihaki, nasi tumeketi, tukitokwa na jasho. Hiyo ni kweli.

¹¹⁷ Ilimbidi Nuhu kutoa jasho pia. Si kubadilisha kutoka kwa Sulemani sasa hadi kwa Nuhu, lakini je, mliona Mungu, baada ya Nuhu kutoa Ujumbe wake, Mungu alimwambia aingie safinani, Naye akamtia muhuri mle ndani, ndipo kesho yake asubuhi akafikiri ingenyesha.

¹¹⁸ Lakini mnajua, Nuhu aliingia mle kwenye siku ya kumi na saba ya Februari, lakini mnajua nini? Haikunyesha kwa juma moja. Nao watu walikuwa wameketi karibu pale, wakasema, “Vema,” mwaminio mkwamia mpakani akasema, “mzee huyo huenda alikuwa sahihi. Hebu tupande twende tuone kama yanakuja, sayansi inasema hakuna maji huko juu, bali alisema ya kwamba Mungu wake angeweza kutengeneza maji huko juu kama Yeye aliliahidhi, kwa hiyo huenda yuko sahihi. Hebu na tukae tu mpakani.”

¹¹⁹ Kuna wengi sana wa namna hiyo siku hizi, kuona tu kitakachotukia, mnaona. Kwa hiyo ninii, kasema, “Kama kweli ikianza, kama vile maji fulani huko juu angani, mawingu, ama chochote kile, tutabisha mlango, na kuingia ndani.”

¹²⁰ Vema, siku ya kwanza Nuhu aliamini itanyesha, kwa hiyo akaketi, na kuchungulia kwenye dirisha hilo, ndipo jua likachomoza, likapita, wala hakuna hata tone la mvua. Mwajua, ndipo Nuhu akaanza kushangaa, “Sijui kama niko sahihi ama nimekosea.” Kwa hiyo basi, siku ya pili ikapita, siku ya tatu ikapita.

¹²¹ Ewe mpentekoste, kamwe isiingie niani mwako kwamba umekosea sasa, keti tu hapo na ultolee jasho. Yeye aliahidi jambo hilo, Naye atalitimiza, mnaona. Naam bwana. Mnaona?

¹²² Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi usiku juu ya *Kudhania*. Vipi kama mitume walisema, “Tumengojea hapa siku tisa, ninaamini tunaye Roho Mtakatifu, nadhani tumempokea. Hebu tuendelee sasa, na tuanze huduma yetu”? Loo, la. Walingojea mpaka ile ishara ya Biblia ilipotokea kule, vema, hiyo ni... mpaka ikawa ni kweli. Halafu hawakuwa wakiwazia chochote.

¹²³ Walimwona Mungu akilithibitisha, wakati Urimu na Thumimu Yake ilipoanza kuangaza maishani mwao, ndipo Petro akasema, “Hili ni Lile lililonenwa na nabii Yoeli.” Hiyo ni kweli, maana alikuwa na Maandiko ya kuliunga mkono. Na hilo ndilo Kanisa la Mungu siku hizi.

¹²⁴ Naye Sulemani alikuwa mtiwa mafuta mkuu wa Mungu. Jinsi ninavyowazia kila mtu katika moyo mmoja na nia moja, taifa zima kwa moyo mmoja na nia moja. Si hivyo ndivyo ilivyopaswa kuwa? Vipi kama makanisa yote yanayoitwa Kanisa la Yesu Kristo, usiku wa leo, yalikuwa tu kama Israeli ilivyokuwa wakati huo, moyo mmoja na nia moja?

¹²⁵ Hakuna hata mmoja aliyeingia na kusema, “Loo, vema, sijui kuhusu maskini Sulemani, sijui kuhusu hilo, ninaamini yeye ni mlokole. Unaonaje kuhusu hilo, Jim?”

“Loo, ninaamini yeye ni mlokole pia.” Watoke, na kuishi chini ya mzeituni wao wenyewe.

¹²⁶ La, kila mtu angekuja mkutanoni, wangesema, “Loo, Mchungaji Sulemani! Sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Utukufu kwa Mungu kwa kutushushia Roho Wake!” Nanyi mwajua, uamsho kama huo huenea kote ulimwenguni, hakika huenea.

¹²⁷ Na sasa, katika siku hizo hawakuwa na televisheni, na—na radio, na magazeti, na kadhalika kutangaza habari, ilikuwa tu ni kutoka mdomo kuingia sikioni. Na ile misafara mikubwa ya ngamia na kadhalika ikipitia sehemu mbalimbali za nchi, mbona, wangeitangaza hiyo habari.

¹²⁸ Ndipo baada ya kitambo kidogo ikafika huko chini *sana* Sheba, huko chini kabisa. Basi kulikuwako na maskini malkia mmoja kule chini, sasa, alikuwa ni kafiri, lakini akaanza kumsikia mtu mmoja akiingia na kusema, “Loo, ndiyo kwanza nipiitie Israeli, nasi tukachukua bidhaa huko juu na tukazileta huku chini. Na, loo, mnapaswa kuiona nchi hiyo! Mnapaswa kuona ni mputano wa namna gani wanaouendeleza kule juu. Wao ni mtu mmoja tu.

¹²⁹ “Nanyi mwajua wana Mungu huko juu ambaye wanamwita Yehova, na kwamba Yehova amejichagulia Mwenyewe mtu, Naye anajithibitisha Mwenyewe kuwa Yehova kupitia kwa mtu huyo.” Mnaona? Loo, jamani! Hapana shaka yalikuwa mazungumzo mazuri.

¹³⁰ Mnajua, imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo watu hawa wakisema hivyo, huko chini kabisa moyoni mwa maskini malkia huyu, akaanza kushangaa, “Sijui kama hayo yote ni kweli. Vema, ngoja mpaka msafara mwingine wa ngamia utakapopita.” Na kwa hiyo, huo mwingine ukaja. “Je, wewe umepitia Israeli?”

“Naam, nimepitia huko.”

“Hiyo ni kweli, ati wana uamsho kule juu, Pentekoste, ama, ninii . . . ?” Vema, Pentekoste ya siku hiyo, mnaona. “Wana uamsho halisi?”

“Loo, wana moyo mmoja na nia moja.”

¹³¹ “Loo, jamani!” Laiti kundi hili lingeweza kuwa hivyo, usiku wa leo. Nawaambia, Columbia ingekuwa na vichwa vyahabari asubuhi, kwenye gazeti, nawaambia hivyo.

“Naam, naam. Ajabu!” Kisha kasema, “Loo, naam, hilo!”

“Hebu niambie, ulimwona yule mtu waliye naye kule juu, Sulemani?”

“Naam.”

“Je, ni kweli kwamba wana Mungu anayejitambulisha Mwenyewe kupitia kwoo?”

“Naam, hiyo ni kweli.”

¹³² Jamani, maskini moyo huo ukaanza kupiga, alitaka kwenda. Sasa, nafikiri kama tunganeanza kusimulia jinsi watu wetu walivyokuwa wazuri, jinsi huyu Roho Mtakatifu alivyo wa ajabu, badala ya kujaribu kusukumana chini, mnaona, mmoja kwa mwingine, nafikiri ingefanya kila . . . Ninyi ni chumvi ya dunia, mnaona, bali chumvi inaweza tu kuokoa inapogusa. Mnaona? Kwa hiyo nafikiri kama tukikolea chumvi sana, ulimwengu ungeona kiu sana. Hivi hamwoni hivyo? Hiyo ni kweli, koleeni chumvi sana.

¹³³ Na sasa, tunaona ya kwamba Sulemani alikuwa tu na wakati mzuri sana. Na kwa hiyo maskini malkia huyu akaanza kuona

njaa na kiu. Nami ninawazia tu angeamka usiku, naye angewaita wasichana wa—wa—wake, naye angesema, “Loo, niliota ndoto, nami nikaota ya kwamba mimi... kwa namna fulani ndoto ya ajabu. Nami ninaamini ya kwamba labda ilikuwa ni kwa sababu kiongozi huyo wa kundi hilo leo alikuwa akiniambia kuhusu uamsho huo huko Israeli.”

¹³⁴ Hatimaye moyo wake ukaanza kudunda, hata akasema, “Vema, mwajua, nitapanda kwenda kujionea mwenyewe.” Hilo ni zuri. Fanya chaguo lako. Unajua wakati kitu fulani kinapoanza kupiga, kinapoanza kuona kiu, ni wakati wa kwenda kuwinda basi. Ukianza kuwazia, “Huenda nikafa moja ya siku hizi. Simjui Mungu,” afadhali uanze, maana hiyo ni taa nyekundu ya Mungu, ile selo inashushwa, kwa hiyo afadhali uharakishe.

¹³⁵ Kama kitu fulani kikikwambia, usiku wa leo, “Ninaamini kuna chemchemi ya uponyaji mahali fulani.” Ishara ya Mungu ikilia, ingia, upesi sana. Maji tayari yametibuliwa, yote unayopaswa kufanya ni kuingia moja kwa moja.

“Yalitibiliwa lini, Ndugu Branham?”

¹³⁶ Miaka elfu moja mia tisa iliyopita pale Kalvari, ile shida. Kisha kwenye Siku ya Pentekoste, kweli kitu hicho chote kilitibiliwa, kweli kilitibiliwa wakati huo. Sasa, yote unayopaswa kufanya ni kuingia moja kwa moja kwenye maji ya Roho, upate kuponywa.

¹³⁷ Sasa, maskini mwanamke huyu, alikuwa akiona njaa na kiu ya kwenda kule. Kwa hiyo sasa, hata hivyo, ye ye alikuwa ni mfuasi wa kanisa, kwa hiyo ilimbidi kwenda kupata kibali kutoka kwa kasisi wake mpagani, aone kama angeweza kuhudhuria huo uamsho ama la. Na kwa hiyo ninaweza kumwona sasa akishuka, naye akasema, “Baba Mtakatifu...” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “...Ningetaka kuomba ruhusa kutoka kwako, kama ningeweza, wana uamsho huko Israeli, wananiambia, wanaye Mungu kule ambaye, loo, Yeye anaishi moja kwa moja ndani ya watu, nao wote wana moyo mmoja. Nao wananiambia ya kwamba mtu huyo ana ka-karama ya upambanuzi wa namna fulani, anajua siri, na anaweza kutabiri mambo yatakayotukia. Nao wanasema Mungu huyu mkuu huko juu wanayemtumikia... Nawe wajua, Baba Mtakatifu, ningetaka kushuka kule chini nione kama hiyo ni kweli.”

Ninaweza tu kuwazia kilichotukia, Ninaweza kumsikia akisema, “Mtoto wangu, ati hadhi ya malkia ingeomba kwenda mionganoni mwa kundi kama hilo!”

¹³⁸ Mnajua, mahali Mungu anapomimina Roho Wake, daima wanadharauliwa kwa namna fulani, kama kundi la wasiojua chochote. Hakika hawajui lolote la ulimwengu huu, wanapoteza

nia zao wenyewe, kusudi wapate nia ya Kristo. Mnaona? Na kwa hiyo hapo bila shaka lilikuwa ni bayo, lilinenewa maovu.

¹³⁹ Ninaweza kumsikia akisema, “Mtoto, la hasha! Kama kulikuwa na kitu kama hicho kikiendelea kama—kama karama ya namna hiyo, kingekuwa kanisani mwetu hapa.” Mnajua hilo lingali linaendelea, hakika linaendelea. Kasema, “Mbona, hakika,” kasema, “lingekuwa papa hapa mionganini mwetu ka—katika makundi yetu, hapo ndipo hayo yangekuwa yakiendelea.”

Akasema, “Lakini Baba, si—sivyo ilivyo. Nao wananiambia . . . Kwa hiyo ningetaka tu kupata ruhusa kutoka kwako, kama ningeweza kwenda huko juu.”

¹⁴⁰ “Sikiliza, wewe ni mtu mashuhuri, una sifa nydingi, na wewe ni—wewe ni mtu mashuhuri, huwezi kujidhili mwenyewe kwenda mionganini mwa kundi kama hilo.”

¹⁴¹ Na kwa hiyo, akasema, “Lakini unajua, Bwana, ni—ninataka kwenda kwa vyovyote vile.” Unajua, kuna jambo fulani kulihusu, Mungu anapoanza kuuvuta moyo wako, karibu hakuna kitukachokuweka mbali nalo. Hiyo ni kweli.

Kwa hiyo likaanza kuuvuta moyo wake, mwajua, “Lazima uende kwa vyovyote vile.”

“Vema,” akasema, “nimesikia habari zake,” hivyo ndivyo imani huja, “hebu niende tu nikajionee mwenyewe, nitarudi na kuwalettea ripoti.”

¹⁴² “Hutapata kibali changu kamwe. Mbona, maskini nyanya yako aliyekufa, na mama wa nyanya, na kadhalika, kama malkia waliokutangulia, wangepinduka huko nje makaburini mwao, kama walijua ulifanya jambo kama hilo!”

Ninaweza tu kuwazia maskini moyo wake ukisema, “Vema, afadhalii wajitayarische kupinduka, maana ninaenda,” mnaona. Kwa hiyo . . .

¹⁴³ Kwa nini? Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno. Na hapo Mungu anapoanza kuuvuta moyo, hakuna njia ya kuliiondoa, nenda tu ukatekeleze yale anayokwambia ufanye. Hiyo ndiyo njia pekee ya kufanya jambo hilo. Kwa hiyo huyu hapa, akiuvuta moyo wake, na kuenda . . .

Akasema, “Sasa, angalia, sasa, wewe kaa tu hapa kanisani mwako, na siku moja labda Dagoni mkuu, ama mmoja wa miungu wetu hapa, atajongea.”

¹⁴⁴ Akasema, “Sikiliza hapa, ninataka kukwambia jambo fulani. Nimeishi maisha yangu yote katika hekalu hili, na siku zangu zote umezungumza juu ya mungu fulani, nami nilimsikia mama yangu akisema jambo lile lile, nanyi mna kitabu cha sheria hapa, na mna sanamu zinazoning’inia hapa, wala sijaona jambo moja likitukia.”

¹⁴⁵ Hapo, hilo ndilo ninalopenda. “Na kama kuna kitu kama Mungu kinachoweza kuingia ndani yako...” Je, nyote mnajua utaratibu wa ibada ya kipagani? Ninajua... Sitaki kuninii... Ninaangalia ile saa ya ukutani *pale* juu, nami nitakosea kwenye *hii*.

¹⁴⁶ Kwa hiyo sasa, ibada ya kipagani, jinsi wafanyavyo, wanaileta sanamu na kuisimamisha. Ndipo basi wanamleta kasisi, na kuubariki mshumaa, kisha wanaweka mshumaa huu mbele ya sanamu, nao wanamletea chakula, ndipo wanakula ushirika pamoja naye. Kisha wasasujudu mbele ya sanamu hiyo, na kuyatoa tu mawazo yao hivi kwamba, mpaka wanaamini ya kwamba wanaweza kuisikia sanamu hiyo ikiwajibu. Sasa, hiyo ndiyo ibada ya sanamu, ya kipagani.

¹⁴⁷ Sasa, hilo ni kinyume na Mungu. Mnaona? Mungu si sanamu, Mungu ni Roho, nasi tunasujudu mbele ya Huyo, wala Roho haingii sanamu fulani, kama vile baadhi ya *wanaojiita* Wakristo wangetutaka tuamini, bali Roho anaingia ndani yako, nawe ndiwe nyumba ya Mungu, mausia yaliyo hai, ukitembea huku na huku, ukimdhahirisha Mungu aliye hai. “Kwa maana Mungu hakai katika mahekalu yaliyofanywa kwa mikono. Lakini mwili umeniwekea tayari.” Mnaona?

¹⁴⁸ Wewe ni barua ya Mungu, waraka ulioandikwa, Mungu yuko ndani yako, akijidhihirisha Mwenyewe kukupitia wewe. Kama ungeweza kusujudu mbele za Mungu, na kusema, “Mungu, mimi ni mwenye dhambi, ingia ndani yangu,” halafu Roho Mtakatifu aingie, ndipo basi wewe ni sanamu iliyo hai ya Mungu, mwakilishi aliye hai wa Mungu, ukitembea huku na huku na Mungu akinena kupitia midomo yako na ya wengine.

¹⁴⁹ Sasa, maskini mwanamke huyu anamwambia, labda, kuhani huyu, kasema, “Nimekuwa hapa miaka hii yote, umezungumza juu ya haya yote, sijaona hata wakati mmoja ilinena, sijaona mtu mmoja aliyetenda vyovyote tofauti, daima imekuwa ni kitu kile kile, wala hakuna Uhai ndani yake hata kidogo. Basi endapo kuna mahali ambapo kuna Mungu anayeweza kutoa Uzima, ninautaka.”

Ninasema, “Amina,” kwake. Naam, bwana. “Ninataka kumwona.”

¹⁵⁰ Vema, jambo la kwanza basi, ilimgharimu, uanachama wake. Kwa hiyo akachukua uanachama wake chini ya mkono wake, kwa hiyo nafikiri labda huenda alishuka barabarani akaenda. Sasa, maskini mama huyo alikuwa na mambo ya kumkabili, na sasa, kwenda kule juu.

¹⁵¹ Basi sasa, jambo la kwanza, alisema, “Ninaenda huko juu. Nami nimesoma Vitabu vyote juu ya jinsi Yehova huyu anavyopaswa kuwa, nami ninapanda kwenda kujionea mwenyewe.” Halafu basi, akawapakia ngamia wachache pamoja na zawadi. Naye akasema, “Kama ndivyo ilivyo, basi

nitaiunga mkono. Kama sivyo, nitarudisha pesa zangu.” Jamani, angeweza kuwafundisha baadhi yetu huku Marekani masomo fulani, sivyo? Naam, bwana. Iwapo kuna chochote kwake, inastahili kila kitu; kama sivyo, haifai chochote, iondokee.

¹⁵² Naye akasema, “Ikiwa kitu hiki ambacho Yehova anadai kuwa, kama Yeye amejidhihirisha Mwenyewe, nami ninaweza kuliona kwa macho yangu mwenyewe, basi niko tayari kumtolea kila kitu. Lakini kama sivyo, ninaweza tu kurudisha zawadi zangu.” Sasa, kumbukeni, akiwa na dhahabu hiyo yote na kadhalika juu ya hao ngamia, alikuwa na safari ya mamia ya maili, na mwajua nini? Watoto wa Esau walikuwa nyikani, nao walikuwa ni wanyang’anyi. Na ingekuwa ni mawindo rahisi jinsi gani, akiwa na pesa hizo zote, kwa ku—kundi tu la hao wanyanganyi kumshambulia maskini mama huyo na kumwua yeche pamoja na hao walinzi wachache, matowashi, aliokuwa nao, na kuchukua pesa hizo.

¹⁵³ Lakini mnajua kitu fulani? Unapotoka kwenda kukutana na Kristo, na umeazimia kukutana na Kristo, hakuna hatari unayofahamu hata kidogo. Hujali kitu chochote kingine, una lengo moja na fanaka moja, na hiyo ni kukutana na Kristo. Loo, laiti ulimwengu ungeanza kuona njaa namna hiyo! Alitaka kukutana na Kristo, na hilo lilikuwa ndilo kusudi lake kuu, ama, kukutana na Sulemani, ile karama, na kuona kama ilikuwa ni Mungu. Naye hakujuu hatari yoyote, hakujuu.

¹⁵⁴ Mtu fulani alisema wakati mmoja . . . Nilimwona mwanamke akisimama na kuanza kupaza sauti, naye akakimbia huku na huku, kwa kweli, aliruka kama viti vinne hivi, ndipo baadhi yao wakasema, “Ilionekana kana kwamba mwanamke huyo angelivunja shingo yake.”

¹⁵⁵ Nilimjua, alikuwa maskini mke wa nyumbani wa kawaida kule chini, lakini nikasema, “Hakuwa akiwazia hilo. Alikuwa tu ndio kwanza amevuka, wala asingeweza kuketi chini, hivyo tu. Alikuwa akikimbia, alikuwa anawaka moto.” Nikasema, “Ilimbidi tu kutimua mbio.” Na kwa hiyo, hakuwa anawazia juu ya hatari, alikuwa anaendelea.

¹⁵⁶ Kama vile ungesema, “Vema, sasa, kama hutanimii—kama hutafanya *hivi na vile* na *hivi-na-vile*, utakufa.” Huoni hilo, unaliamini Neno la Mungu kwa ajili yake, nawe unaendelea tu kukimbia. Naye ilimbidi kuendelea.

¹⁵⁷ Na sasa, kumbukeni, ukitoa kwenye ninii yako, uangalie kwenye ramani yako, kutoka mahali Yerusalem ilipokuwa, kote kote mpaka Sheba, hiyo ni kuvuka jangwa la Sahara, na inachukua tu ngamia miezi mitatu kuvuka kule. Sasa, hakuvuka kwa Kadilaki iliyoyoyozwa. Mnaona? Ilimbidi kuvuka juu ya ngamia, nayo ikamchukua miezi mitatu kufanya hivyo. Sasa, hapo ndipo alipokuwa akimwonea Mungu njaa kweli.

¹⁵⁸ Shida yetu sisi Wapentekoste, siku hizi, kila kitu kimewekwa mkononi mwetu, nasi tunakiangalia tu, na kusema, "Vema, nadhani ni sawa. Mnaona? Hilo ni zuri sana." Lakini inapokubidi kulipa gharama kama hiyo, unaifurahia kweli unapoipata. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁹ Huyo hapo. Alikuwa, ilimbidi kuvuka Sahara, nayo hii hapa, nao maskini ngamia hawa, labda, wanasaifiri usiku, wajakazi wachache pamoja naye, na kundi la maskini matowashi huko nje, bila kufikiria kitu kingine chochote, lakini siku nzima, ameketi mahali fulani kwenye oasisi, akisoma hayo Magombo, kile Yehova alichokuwa, maana imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu. Alikuwa amechukua Magombo haya na alikuwa akiyasoma, alitaka kujua hasa kwamba Yehova alikuwa nini, naye Sulemani alikuwa akimdhimirisha Yehova, kwa hiyo akaenda akaone.

¹⁶⁰ Vema, hatimaye akawasili, naye akafika langoni. Alipofika langoni, aliwapakua mizigo ngamia wake wote, na labda akawaagesha huko nje uwanjani. Basi hebu tufanye mchezo mdogo wa kuigiza sasa. Ninaweza kuwaona watu kutoka kila mahali pande zote. Ndipo kesho yake asubuhi akajinadhifisha na—na akaenda kwenye m—mkutano, naye akaketi chini, na muda si muda mwajua, Mchungaji Sulemani akatokea, na muziki wote ukapigwa, na kadhalika, ndipo Mchungaji Sulemani akatokea.

¹⁶¹ Alimpata, hakuwa na kadi ya maombi, kwa hiyo alingojea tu huko nyuma kabisa ya jengo, mwajua, kwa hiyo akangojea huko nyuma kwa muda mrefu. Ndipo Mchungaji Sulemani alipoanza ku—alipoanza kuzungumza, wao... aliona ya kwamba hakukuwako na kitu ila hekima ya yale aliyokuwa amesikia.

¹⁶² Ndipo kesho yake asubuhi, alipoingia, nakisia aliketi karibu katikati. Na muda si muda mwajua, ikawa kwamba alijongea karibu kabisa. Ndipo asubuhi moja akaingia mstarini, na akasimama mbele ya Sulemani, akasema, "Sasa, nitaona jinsi, kama ni kweli ama si kweli. Mimi ninaninii tu, mimi... Kitu fulani tu kote ndani yangu kinaniambia ni kweli." Nayo Biblia ilisema hapakuwapo na siri yoyote, ila ambayo Mungu alimjulisha Sulemani juu yake. Hiyo ni kweli.

¹⁶³ Ndipo Sulemani alipoanza kuzungumza naye, na kuutambua moyo wake na shauku zake, mnajua alichosema? Alisimama mbele ya watu, hebu mwangalieni maskini kafiri huyu sasa, akasimama mbele ya watu, naye akasema, "Yote niliyosikia ni kweli, na zaidi ya niliyosikia." Loo, alikuwa ameshawishika maradufu, maana alikuwa ameona kama hao wengine walivyokuwa wameona, na sasa ilikuwa ikifanya kazi kwake. Amina.

¹⁶⁴ Na kama huamini kwamba Roho Mtakatifu ni sahihi, mpe jaribio lilo lilo. Huenda ukamsikia kwa wengine, lakini ngoja mpaka atakapoanza kufanya kazi juu yako mara moja, ndipo utajua hakika ya kwamba ni Karama ya Mungu. Inaondoa hasira yote, dhambi yote, kutokuamini kwote, mashaka yote, hofu zote, hata hofu ya mauti inakuondokea wakati Roho Mtakatifu anapoingia. Loo, ni halisi, enyi marafiki. Kama hujawahi kumpokea, usiache usiku upite bila kumpokea.

¹⁶⁵ Lilikuwa ni—ni jambo kubwa jinsi gani! Maskini mama huyo alisisimkwa sana, mpaka a—akasimama pale, na hata alitaka ku—kuchukua ardhi kidogo arudi nayo. Alifanyika mwaminio kabisa.

¹⁶⁶ Naye Yesu alisema, “Malkia wa Kusini atasimama katika Hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa, kwa kuwa alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu unaojulikana wa siku hizo, mgongoni mwa ngamia apate kusikia hekima ya Sulemani, nami nawaambia ya kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.” Kwa kuwa Sulemani alikuwa akipambanua, angalia jinsi hilo lilivyokuwa kubwa zaidi.

¹⁶⁷ Na sasa, usiku wa leo, baada ya Yeye kufa, kuzikwa, na kufufuka tena kuingia Utukufuni kama Kuhani Mkuu kwa miaka elfu mbili, nao ulimwengu wa kikafiri, uliovuviwa na ukomunisti jinsi ulivyo usiku wa leo, katikati ya hayo yote, aliye mkuu kuliko Sulemani amesimama hapa, aliye mkuu kuliko wote, Mungu yeye yule aliye na karama ile ile iliyoahidiwa, Roho Mtakatifu yeye yule aliye na Uzima wa Milele.

¹⁶⁸ Maskini mama huyo alikuwa na shida gani? Alikuwa ameona kitu fulani kwa wakati mmoja maishani mwake ambacho kilikuwa halisi, kitu ambacho hakikuwa ni cha kuigiza, desturi, ama taratibu ya kitu fulani. Alikuwa amekuja kanisani ambako aliona Mungu aliye hai akitenda kazi. Sasa, kama maskini mwanamke huyo atasimama katika siku ambayo Yesu alikuwa duniani pamoja na kizazi hicho na kukihukumu kuwa kimekosa, viyi kuhusu siku hizi?

¹⁶⁹ Wakati alipokuja yapata siku elfu mbili, loo, la, siku tisini, sijui ilikuwa ni maili ngapi, iko huko chini kabisa, nililiwazia wakati mmoja, lakini najua inachukua muda mrefu kufika kule juu, yapata—yapata siku tisini kufika kule, miezi mitatu kuititia jangwani kuisikia hekima ya Sulemani, na hapa Marekani ni vigumu kwetu kuvuka barabara kuona nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo, kwa Biblia, Urimu na Thumimu, iliyoahidi ya kwamba ingemwakisi Yeye katika siku za mwisho, na hili hapa kwa ushahidi wa Biblia.

¹⁷⁰ Roho Mtakatifu, pamoja na ushahidi wa Biblia, amekuja Kanisani, na kuonyesha ishara na nguvu za Yesu aliyefufuka moja kwa moja mionganoni mwetu sasa, aliye mkuu kuliko

Sulemani. Roho wa Mungu asiyepatikana na mauti anatenda kazi, si na mmoja tu, Yeye anafanya kazi katika Kanisa zima, akionyesha ishara na maajabu, akiwaponya wagonjwa, akiwafufua wafu, kutoa pepo, kunena kwa lugha, kutoa tafsiri, kumimina nguvu, kuwaongoa wenye dhambi, loo, Yeye anaonyesha ishara za kuwepo Kwake hapa, akiipambanua mioyo na mawazo ya watu ambalo aliahidi atafanya. Pia kumbukeni, ishara ya mwisho ambayo Israeli walipata ilikuwa ni hiyo, na hiyo ndiyo ishara ya mwisho iliyoahidiwa sasa, ishara ya siku za mwisho, nasi tumewasili.

¹⁷¹ Maskini Malkia huyo alikuwa ameona kitu ambacho kilikuwa halisi, kitu ambacho angeweza kukiangalia mwenyewe, na kilikuwa ni halisi, angeweza kuona jinsi kitu hicho kiliyyofanya juu ya mwanamume huyo. Alijua ya kwamba kilikuwa ni kitu ambacho . . .

¹⁷² Watu siku hizi, ninaamini kama Kanisa, kama nilivyosema, lisingepulizia mvuke mwingi sana kwa filimbi, bali lingeuweka kazini, na kuona njaa na kiu ya kuwapeleka watu mahali ambapo mambo kama hayo yanaendelea . . . Mnaona? Wanataka kuona kitu halisi, hawataki tu kuingia, na kuandika jina lao kwenye kitabu. Watu walio na njaa na kiu ya Mungu wanakuja kupata kitu halisi.

¹⁷³ Ninakumbuka si muda mrefu uliopita, huenda niliwaambia jambo hili dogo, kama mjuavyo, mimi ni mwindaji, ama, ninapenda tu kuwinda, mimi si mwindaji, bali ninawindia Afrika, India, na kila mahali kote ulimwenguni. Mama yangu alikuwa chotara, naye . . . naye babu yangu alikuwa mwindaji mashuhuri, na kwa hiyo sikuzote nilikupenda.

¹⁷⁴ Kitu cha kwanza nilichopata kununua, niliangusha mimea ya viazi vitamu siku nzima nikapata robo, nikajinunulia mitego miwili ya chuma, ndipo nikaanza biashara. Nami nikajinasia oposamu na kuiiza ngozi hiyo, ndipo nikajinunulia mitego mingine, nami nikaingia katika biashara halisi basi, hiyo ilikuwa ni yapata umri wa kama miaka minane, nami nimekuwa nikiwinda tangu wakati huo.

¹⁷⁵ Sasa, nilikuwa nikienda kwenye misitu ya kaskazini na kuwinda, huko mbali kaskazini. Nami nilikuwa nikiwinda pamoja na mwindaji hodari kule juu, jina lake Bert Call, ambaye alikuwa mwindaji hodari, haikunibidi kumhofia. Mara nyingi unampeleka mtu mwituni, na usipoangalia, kama kweli hajui mielekeo, na jinsi ya kusoma ishara, kuvu kwenye miti, na kadhalika, itakubidi kumtafuta kwa siku moja au mbili, anageuzwa, huko nje tu kidogo kidogo. Lakini sio Bert, na hiyo nchi tambarare huko juu karibu na Maine na kadhalika, yeye alijua mahali alipokuwa. Tungeenda kuwinda asubuhi moja, naye, isingekubidi kuwa na wasiwasi, kama tungetengana, yeye,

Bert angekuwa huko usiku huo, hivyo tu. Na kwa hiyo tulipenda kuwinda pamoja.

¹⁷⁶ Kulikuwa na jambo moja tu dhidi ya Bert nililokuwa nalo, nalo lilikuwa kwamba alikuwa ndiye mtu katili sana niliyepata kuona. Alikuwa na macho kama tu ya mjusi, mwajua, moja kwa moja nyuma, kama vile baadhi ya wanawake hawa wanavyojaribu kupaka macho yao rangi siku hizi za mwisho, mmewaona, kitu hicho kinachoonekana cha kuchekesha, haionekani kama mwanadamu wa kawaida. Naye kwa namna fulani alikuwa na macho yaliyoelekea upande, yanayoonekana kama ya mjusi, naye alikuwa katili.

¹⁷⁷ Nanyi mwajua, alikuwa akienda pamoja nami kuwinda, naye ange—angewapiga risasi hao watoto wadogo wa kulungu ili tu kunifanya nijisikie vibaya. Nami nikasema, “Bert...” Sasa, ni sawa, sina neno dhidi ya kumwua mtoto wa kulungu, sasa, kwenu ninyi ndugu wawindaji, mnaona. La, bwana, kama jimbo linasema unaweza kumchukua, vema, maana hifadhi huliangalia hilo kuona kama wana wa kutosha, wanaweza kuliachilia hivyo.

¹⁷⁸ Wala hakuna ubaya katika u—umri wa mnyama, Ibrahimu alimwua ndama, naye Mungu akamla. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo msifikirie ujana, ila tu kuwa katili, ndivyo hivyo. Kufanya hivyo tu upate kuwa katili, nafikiri hayo ni mauaji tu, wala nisingeua kitu chochote namna hiyo. Na kwa hiyo, Bert angeninii tu, angemwona mtoto wa kulungu akikimbia, naye angemwangusha tu, namna *hiyo* na kusema....

Nami ningesema, “Bert, ninakupenda, wewe ni mtu mzuri, lakini wewe—wewe ndiye mtu katili sana niliyepata kumwona.”

Akasema, “Aa, mhubiri, hivyo ndivyo mlivyo ninyi jamaa, nyinyi ni waoga kupindukia.” Akasema, “Rudia fahamu zako.”

¹⁷⁹ Basi nikapanda huko wakati mmoja wa majira ya baridi kali, nikaenda kuwinda pamoja naye, ilikuwa kidogo mwishomi mwa msimu wa kupukutika, na kulikuwa na namna fulani ya theluji iliyokuwa tayari imeanguka, nao msimu wa kuwinda ulikuwa umeendelea kwa majuma kadhaa. Nami...Bert alikuwa, alipanda huko juu kunilaki, nasi tukafika kambini. Ndipo tukachukua chokoleti yetu moto, tungeiweka kwenye chupa yetu ya themosi. Ndipo basi, tukatoka, tukashikwa mahali fulani kwenye theluji, wala tusingeweza, litubidi kukaa usiku kucha, tukawasha moto, mbona, tungekunywa chokoleti moto kutudumisha tukiwa na joto kwa namna fulani usiku kucha, na labda sambusa, ama chochote kile, na—na sikuzote tulibeba viberiti vikavu kuwashaa moto.

¹⁸⁰ Basi asubuhi hiyo tulipitia kwenye unjia wa Jefferson, na kuwingia kwenye Safu ya Milima ya Rais. Na kwa hiyo, tukaenda...Hakuna hata mburuzo, hao kulungu wadogo wenye mikia myeupe, mnazungumza kuhusu Houdini kwamba ni

bingwa wa kutoroka, wao ni hodari kweli. Nao wanaweza kuingia chini ya hivyo vichaka, nawe utaninii, hutawaona. Moja kwa moja jioni sana kabla ya giza kuingia utamwona mmoja akisogea tu, ikiwa ni mbalamwezi, atangojea mpaka usiku aje ale. Na wakati, baada ya kurushiwa risasi, kwa vyovyote vile, ni vigumu sana, sana kuwapata. Wala hata hatukuwa tumepata mburuzo mmoja asubuhi hiyo, basi ikafika yapata adhuhuri, na kabla hatujaondoka, Bert akasema, “Nina kitu kwa ajili yako, Billy.”

Nami nikasema, “Ni kitu gani?” Ndipo akaingiza mkono mfukoni mwake, naye alikuwa na filimbi ndogo. Nikasema, “Ni kitu gani hicho? Mbwa mwitu, kwa ajili ya mbwa mwitu?”

¹⁸¹ Akasema, “La,” kasema, “huo ni mlion wa kulungu.” Kasema, “Hebu sikiliza hii,” naye akaipuliza. Nanyi mmesikia m—mtoto wa kulungu akilia, kama kulungu mdogo, mtoto wa kulungu, akimlilia mama yake.

Nami nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

Akasema, “Loo, Mhubiri,” kasema, “ninyi jamani,” kasema, “ninyi ni waoga kupita kiasi kuwa wawindaji.”

Nami nikasema, “Vema, Bert, napenda kuwinda.” Na kwa kweli, imenilazimu kumwulia kulungu wake mara nyangi.

Lakini akasema—akasema, “Lakini ninyi watu ni waoga kupita kiasi.”

¹⁸² Nikasema, “Vema, usiwapige risasi hao jamaa wadogo, Bert.” Nikasema, “Hupaswi kufanya hivyo.” Naye... Nikasema, “Hutapiga filimbi hiyo namna hiyo.”

Akasema, “Wewe angalia tu.”

¹⁸³ Vema, nilikuwa nimesahau jambo hilo. Ilikuwa yapata saa tano mchana, nasi tukafikia mahali pakubwa kama chumba hiki humu ndani, theluji ardhini, palikuwa ni mahali wazi. Ndipo maskini Bert akaketi chini, akaanza kunyosha mkono namna *hii*, nilifikiri alikuwa anataka kunywa chokoleti yake moto. Kwa hiyo akaunyosha mkono namna *hii*, na alipofanya hivyo akatoa maskini filimbi *hii*. Nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

Kasema, “Shh!” Alichukua filimbi hiyo ndogo, akalia, ilisikika kabisa kama mtoto m—mdogo, wa kulungu akimlilia mama yake.

¹⁸⁴ Basi alipofanya hivyo, upande wa pili tu wa huo uwazi, jike mkubwa akasimama, sasa, huyo ni mama kulungu, masikio hayo makubwa mno, macho makubwa ya hudhurungi, mnyama wa kupendeza. Naye akaangalia... Maskini Bert akainamisha kichwa chake chini ya kichaka hiki kidogo, hayo macho ya mjisui yakaniangalia, mwajua, nami nikawazia, “Loo, jamani! Hakika hatafanya hivyo.” Naye akaipuliza tena.

¹⁸⁵ Sasa, hilo si la kawaida, wakati huo wa mchana, kwa kulungu kuinuka, hasa sana katika msimu wa kuwinda. Basi wakati alipoipiga tena, akatoka moja kwa moja kwenye uwazi huo. Sasa, hilo si la kawaida sana wakati wowote, kwao kufanya hivyo, lakini mwajua, ye ye alikuwa ni mama, na ndani ya moyo wake alikuwa ni mama. Hakuwa akijionyesha kwa kitu chochote, kwa kweli alizaliwa mama, na mtoto mchanga alikuwa taabani, naye hakuogopa chochote wakati huo, alitaka kujua mahali mtoto huyo alipokuwa. Nami bado ninaweza kuyaona hayo masikio makubwa, yakinkeza tu namna *hiyo*, mnajua jinsi yanavyofanya, kichwa hicho juu namna *hiyo*.

¹⁸⁶ Mara nikamwona Bert... Hatuweki ganda kwenye mtutu, ama, ganda, mpaka uone kitu cha kupiga risasi, kwa hiyo akaingiza ganda, naye alikuwa na .30-06. Niliona... Loo, alikuwa hodari wa shabaha. Nami nikamwona akilenga namna *hiyo*, ndipo nikawazia, “Loo, jamani, ataulipua huo moyo wake mwaminifu moja kwa moja kupitia kwake.” Mnaona? “Angeweza je kufanya hivyo, huku huyo mama anajaribu kumtafuta mtoto wake?” Mnaona?

¹⁸⁷ Naye akaipiga tena. Naye yule—yule kulungu akatambua, alipopata harufu, mwindaji alikuwa pale. Lakini mnajua, hakuruka kamwe, kwa kawaida angeruka, lakini mtoto huyo alikuwa akilia kwa huzuni sana, hata hakujali kama ilimaanisha kifo, alikuwa anaenda kumtafuta mtoto huyo aliye taabani. Huo ni umama halisi wa kweli, hakuna kitu kitakachopachukua mahali pake, ni vigumu, Mungu pekee.

¹⁸⁸ Mungu alisema, “Je, mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya? Naam,” kasema, “huenda akamsahau mtoto wake mchanga, lakini sitawasahau kamwe, kwa kuwa majina yenu yameandikwa katika vitanga vya mikono Yangu.”

¹⁸⁹ Kwa hiyo nikamwangalia mwindaji huyo, naye akageuka, na kuilenga bunduki hiyo chini. Nami nilijua ya kwamba hiyo shabaha ilikuwa moja kwa moja kwenye moyo wake, risasi hiyo kubwa ya kizio mia na themanini ya uyoga, ingeulipulia mbali moyo huo mwaminifu wa mama huyo.

¹⁹⁰ Nikawaza, “Anawezaje kufanya hivyo?” Nisingeweza kuiangalia. Nikageuza tu mgongo wangu *hivi*. Sasa, kwa namna fulani niligeuka, nilikuwa nyuma ya vichaka fulani, Nilisema tu moyoni mwangu, “Baba wa Mbinguni, usimwache afanye hivyo. Usimwache afanye hivyo.” Nami, kwa nafsi yangu tu, nilikuwa tu nikisikiliza wakati wowote kusikia mlio huo wa bunduki, nami nikaona haikupiga. Nikangojea kwa dakika moja zaidi, nayo haikupiga, ndipo nikageuka kuangalia, nao huo mtutu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*.

¹⁹¹ Nami nikamwangalia, naye akageuka, hayo machozi makubwa mno yalikuwa yakinkeza mashavuni mwake. Akaitupa hiyo bunduki chini, akasema, “Billy, nimetosheka

nayo.” Akanishika kwenye mguu wa suruali, akasema, “Ninataka unionbee na kuniongoza kwa huyo Yesu unayenena habari zake.”

¹⁹² Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa ameona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza, aliona kitu ambacho kilikuwa halisi, aliridhika basi. Mnaona? Hicho ndicho ungetaka kujua, kitu halisi, kitu fulani, si desturi, kujifanya, bali Mungu halisi, upendo halisi, matendo halisi. Si hiyo ndiyo moyo wako unaonea njaa? Na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza Naye kwa dakika moja tu.

¹⁹³ Nashangaa sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kwa muda kidogo tu, wazia tu kidogo, ni wangapi wenu hapa usiku wa leo, sasa, iweni waaminifu, ni wangapi wenu wangetaka kuwa Mkristo wa aina iyo hiyo moyoni mwako, Mkristo kadiri yule kulungu alivyokuwa mama? Inua tu mikono wako, useme, “Ningependa kuwa Mkristo wa namna hiyo.” Mungu awabariki. “Kitu ambacho kingenisukuma moja kwa moja kwenye taya za mauti, nao upendo wangu kwa Kristo ungesonga mbele moja kwa moja, upendo usiokufa. Ninampenda kwa yote yaliyo ndani yangu.” Anaiona mikono yenu.

¹⁹⁴ Baba yetu wa Mbinguni, kweli hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, aliye mkuu kuliko yejote wa manabii yuko hapa, Roho Mtakatifu yupo hapa, Karama ya Mungu kwa ulimwengu. Naye, kwa mamia na mamia ya miaka hangeweza kuingia kanisani, bali katika siku hii ya mwisho Yeye aliahidi ya kwamba angekuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, nasi tunamwona, usiku wa leo, akitenda kazi.

¹⁹⁵ Sasa, Yeye alilingia ndani yetu akinena kwa lugha, alilingia ndani yetu kwa furaha, na sasa anaendelea kuleta karama kubwa zaidi, Naye huwaponya wagonjwa, na sasa amewafufua wafu. Naye huyu hapa, Ne—Neno la Mungu, Yeye ni Neno, Neno lilifanyika mwili. Na sasa Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata linaenda kugawanya mifupa na mafuta yaliyomo ndani yake, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo, Roho Mtakatifu.

¹⁹⁶ Na, usiku wa leo, hadithi hii ndogo kuhusu mimi na Bert, huko juu, Baba . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ishi tu kama walimwengu, nao walimwengu hawawezi kuona tofauti yoyote ndani yao na mwenendo wa walimwengu wengine. Unaweza kumchukua maskini mama kulungu, na kumleta mmoja wa watoto Wako kwenye akili timamu. Asante kwa ajili yake, Bwana.

¹⁹⁷ Nami naomba, usiku wa leo, ya kwamba Roho Mtakatifu ataujaza tu kila moyo kwa upendo na amani, na tuuone mkono wa Mungu wetu, kwa maana kweli, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Na sasa, Wewe uliahidi katika siku za mwisho ya kwamba ungefanya jambo hili, kama ilivyokuwa

katika siku za Nuhu, na kama siku za Sodoma, na ndipo ukawashughulikia Wayahudi na Wasamaria katika siku hiyo, Wamataifa wamekuwa na miaka elfu mbili ya mafunzo.

¹⁹⁸ Na sasa katika wakati wa mwisho, usingeweza kuwa mwenye haki, Bwana, kisha uache... Ilibidi tu Wayahudi waione ishara hiyo na kulazimika kuikataa, ndipo wakakataliwa mbali. Sasa, Baba, kama uliwapa hiyo, na kuwaacha Mataifa waingie kwa theologia peke yake, Wewe si Baba wa namna hiyo, Wewe ni yeye yule, unampa mmoja wa watoto wako sawa na yule mwingine, unawapenda wote. Na kila kizazi, kila kipindi cha wakati, kinapokea ishara yake na karama kwa wakati huo.

¹⁹⁹ Na sasa, Baba, tunajua ya kwamba... Tunashukuru, usiku wa leo, kuwa na ishara ya Roho Mtakatifu, Yesu aliyefufuka akiliweka Kanisa Lake tayari. Tubariki usiku wa leo, tupe Uwepo Wako, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁰⁰ Sasa, huku mioyo yetu Kwake... Nami ninasikitika kwa kuendelea kirefu hivi, kweli nimechelewa kwa nusu saa. Nilimwambia Billy nitakuwa nimeondoka ifikapo saa tatu na nusu, na, ili ndugu waweze kubatiza na kadhalika. Inatupasa kutambaa tutoke asubuhi, yapata saa tisa. Sasa, hilo linanifanya, kuwazia kwamba, linanitia wasiwasi, na hiyo ndiyo sababu ninaukata-kata ujumbe wangu jinsi nifanyavyo, samahani kwa hilo. Lakini ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu amesema jambo fulani moyoni mwako ambalo litakufanya uamini, hiyo ni kweli, kukufanya uamini kwa moyo wako wote.

²⁰¹ Sasa, tungeweza kuita, nafikiri tuna kadi chache za maombi, Tungeweza kuita kadi hizo za maombi hapa juu na kuwaombea, ama tunaweza kufanya vyovyote tutakavyo, kufunga mkutano. Au je, mngetaka tu, kumpa kila mtu nafasi sawa? Hebu na tuombe tu basi, na kumwomba Baba wa Mbinguni, kwamba mtu yeoyote huko nje aliye na imani ya kutosha kumgusa Yeye. Je, mngependa kufanya hivyo? Mtaamini mna imani ya kutosha kufanya hivyo? Inueni mikono yenu. Mnaona? Sisi hapa. Hiyo ni—hiyo ni—hiyo ni kweli.

²⁰² Mnaona, enyi marafiki, mahali ninapojibandika, mnaona, nikijibandika hapa nje? Hii hapa. Kuna watu, siwajui, lakini sasa, ninasema hapa ya kwamba—ya kwamba Mungu anawajua. Nami... Watakapokuja kuona hekima ya Sulemani, halafu wanapokuja kuona kazi ya Yesu...

²⁰³ Sasa kumbukeni, Mungu hawezi kubadilika, Yeye ni Mungu daima. Wakati Mungu anapofanya... Hiyo ni imani yangu katika Biblia, kama Mungu akiwahi kufanya uamuzi juu ya jambo lolote, halina budi kubaki hivyo daima, haliwezi kubadilika kamwe, kwa sababu hawezi leo kuwa na...

²⁰⁴ Kila moja ya maamuzi Yake ni mkamilifu, kwa sababu Yeye hana kikomo. Mnajua maana ya *bila kikomo?* Unajua,

unapochukua kamera yako na kuiweka kwenye *bila kikomo*? Hiyo inamaanisha tu, “tangu wakati huo na kuendelea.” Vema, Mungu hana kikomo. Mnaona? Hapo ndipo neno *bila kikomo* linapokuja.

²⁰⁵ Sasa, Ye—Yeye kamwe hakuanza, kwa hiyo kamwe haishi, na chochote kilichopata kuanza, huisha. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu inatubidi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, tupate kuwa na Uzima wa Mungu ndani yetu, tuwe na Uzima wa Milele, ambaao, neno la Kiyunani Zoe linamaanisha, “Uzima wa Mungu Mwenyewe ndani yetu,” nao Uhai huo hauwezi kufa zaidi ya vile Mungu awezavyo kufa, kwa sababu ni sehemu ya Mungu, Asiyé na kikomo. Hiyo ni kweli. Na huyo ni Roho Wake.

²⁰⁶ Sasa, kama Roho Wake alitenda kazi juu ya wakati wa Sulemani, alitenda kazi katika wakati wa Bwana Yesu, na akalihidi hapa katika siku za mwisho, ni Mungu yeye yule. Amina. Aliahidi jambo hilo. Mnaamini hayo, nyote, sivyo? Mnaamini hilo, ndugu zangu? Hilo ni zuri.

²⁰⁷ Laiti ningaliweza kuwachukua ninyi nyote pamoja nami katika mikutano hii, uungwaji mkono mzuri namna hiyo. Mungu atafanya tu lolote mkiwa na mengi karibu nanyi. Hiyo ni kweli. Nyote iweni na hakika kama nikirudi kwenye msimu huu wa kupukutika, njoni, kila mmoja wenu, mnaona, na tuwe na ushirika tena, tuwe na usiku kadhaa wa mikutano, mpaka wakati huo niombeeni.

²⁰⁸ Sasa, mimi hapa, nimesimama hapa. Ni watu wangapi katika kusanyiko hili . . . ? Sasa, ninamtambua huyo, sina hakika, *huyu* ni Dada Bryant, na watu hawa watatu wanaoketi papa *hana*, najua. Sasa, nje ya hao sioni mtu ye yeyote ninayemjua, ila ndugu huyu papa *hana*. Basi alishuka, alikuwa ni Mbaptisti, akashuka, akaendelea kuzungumza juu ya Roho Mtakatifu na kadhalika. Asingweza kuacha kuvuta sigara, naye akapata mahojiano kadhaa, ndipo asubuhi moja Roho Mtakatifu akashuka moja kwa moja, na huo ulikuwa ndio mwisho wake. Kwa hiyo, akasema, “Mimi, ninaishi huko Carolina, sininii . . .”

²⁰⁹ Nikasema, “Mtafute Ndugu Bigby, jiunge na kanisa lake,” nikasema, “maana hapo ndipo mahali pa kwenda kama wewe . . .” Nikasema, “maana ni—ninajua yeye ni mwalimu halisi, kwa hiyo, na ni mtu wa Mungu.”

²¹⁰ Kwa hiyo sasa, sikuwajua ndugu wengine wengi, lakini nilimjua Ndugu Bigby. Nami najua kuna watu wengine wazuri, nimekutana nao hapa ukumbini, usiku wa leo, nikaangalia juu na chini hapa, na sisi, sisi sote ni watoto wa Mungu, hivyo tu.

²¹¹ Sasa, ni watu wangapi hapa ndani ambaao ni wagonjwa ambaao siwajui nanyi mnataka Mungu awasaidie, nawe unajua ya kwamba sijui lolote kukuhusu, sijui lolote kuhusu shida yako, ama chochote kile? Mnasema, kama ninavyoona, hapa mahali fulani, huenda ilikuwa ni kwenye mkutano huo

mwingine, mwanamke mmoja alipitia jukwaani, kasema, “Naam, ninakujua, nilikuwa kwenye mmoja wa mikutano yako mingine wakati mmoja, miaka minne au mitano iliyopita.”

²¹² Jamani, hebu wazieni tu jambo hilo, ni makumi mangapi ya maelfu nimekutana nao tangu wakati huo, mnaona, sina njia ya kuwajua, ni kupita tu jukwaani, ama kuketi kule kwenye kusanyiko. Basi ni wangapi walio wagonjwa sasa, nanyi mnajua ya kwamba sijui mna shida gani? Inueni tu mikono yenu, popote mlipo. Vema, inaonekana kana kwamba ni kila mahali, na Mungu hakika atatusaidia sasa.

²¹³ Sasa, ninawatakeni mfanye hivi: ninawatakeni mwache kuwazia juu ya sisi wahudumu, ndugu hapa jukwaani. Sasa, hii si huko nyuma kwenye ubao fulani wa ouija, katika chumba fulani chenyenye giza, taa zimezimwa, kazi ya ibilisi, hii ni moja kwa moja hapa nje katika nuru wazi, peupe, katika Uwepo wa Yesu Kristo na Kanisa Lake, Biblia Yake Takatifu imewekwa hapa ikilitangaza. *Hii* ndiyo Urimu, Urimu na Thumimu, *Hii* ndiyo naivera, hiyo ndiyo naivera iliyoinmarishwa ya kila mwaminio. Hiyo ni kweli. Mnaona? Nayu Urimu na Thumimu ni ile ya kimbunguni iliyotoka kwake, ikiitangaza.

²¹⁴ Sasa, amini kwa moyo wako wote. Usitie shaka sasa, ninawatakeni mwamini kweli. Nawe omba na kusema, “Baba wa Mbinguni, ninakushukuru sana kwamba ulimtuma Mwanaao, Kristo Yesu, Yeye alikuwa badala yangu. Tunasema Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa, hayo ni mambo aliyofanya. Ameketi mkono wa kuume wa Ukuu, usiku wa leo, kuniombea ninapokiri.

²¹⁵ “Ndiyo kwanza nimsikie Ndugu Branham akisimulia, katika siku chache zilizopita usiku, ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa kali kuliko upanga ukatao kuwili, Nalo lilikuwa ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo. Sasa, ulipokuwa hapa duniani ulikuwa Neno lililofanyika mwili likakaa kwetu, tunajua hilo, ya kwamba Wewe ulikuwa Neno. Na sasa tunaamini ya kwamba Neno limekuja katika umbo la Roho Mtakatifu kuthibitisha Neno lililoandikwa,” mnaona, “kulifanya sahihi.

²¹⁶ “Sasa, mwanamke mmoja aligusa vazi Lako wakati mmoja, na—naye Mwanaao, Yesu Kristo, akageuka na kumtambulisha huyo mwanamke, na kumwambia, kutokwa kwake na damu. Kipofu mmoja alimsimamisha, na kadhalika, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, tunapoyapitia Maandiko. Na sasa, tunaona ya kwamba Wewe ulisema, ‘Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.’”

²¹⁷ Sasa, hivyo ndivyo alivyosema. Hiyo ni kweli, ndugu? Tunataka kuamini hilo sasa. Hebu sote tuliamini kwa moyo wetu wote, nanyi nyote mniombee.

²¹⁸ Sasa, kila mmoja wenu, ondoeni tu kutokuamini kwenu, mkuweke chini ya miguu yenu, na kukulaani katika Jina la

Bwana Yesu, kisha mlichukue Neno la Mungu, na kulishikilia huko juu, na kusema, “Mimi ni mwaminio, nami ni—nitaliamini kwa moyo wangu wote.”

²¹⁹ Sisemi kwamba atafanya hivyo. Asipofanya hivyo, si—siwezi kumfanya afanye hivyo, mwajua, Yeye ni mwenye haki, Yeye ni Mungu, mnaona, Ni—ni—ninaliamini tu, na sasa, asipofanya hivyo, basi—basi tutaninii, nafikiri kuna walio na kadi chache za maombi humu jengoni, huenda wakawa hapa usiku wa leo, basi endapo wako, vema, tutawaita, na kuwaleta ndugu wahudumu hapa, na kuwaombea. Lakini nafikiri jambo muhimu kwa Mkristo . . .

²²⁰ Mwangalie Mrumi huyo wakati huo. Huyo Myahudi alisema, “Njoo, weka mikono Yako juu ya binti yangu, naye atapona.”

Yule Mrumi alisema, “Ninaamini vyema kuliko hivyo, Wewe sema tu Neno, hivyo tu.”

²²¹ Yesu akageuka na kusema, “Sijaona imani kama hiyo mionganii mwa Israeli.” Mnaona? Hao ni sisi Wamataifa, tunapaswa kujua yale Neno Lake lisemayo, ni kweli. Hiyo ndiyo sababu pekee ya mimi kusimama hapa namna hii usiku wa leo, kwa sababu Neno limeahidi jambo hilo, mnajua hilo. Na, jinsi nimekuwa nikitarajia kwa miaka mingi, jambo fulani kuu litokee katika siku za mwisho, mwajua, tumeahidiwa hilo, ambalo lingileta imani ya watoto iwaelekee wale baba asilia wa Kipentekoste. Hiyo ni kweli. Tunalitazamia, Yeye aliliahidi, nasi tunaliamini.

²²² Sasa, ombeni tu, nami nitaomba pamoja nanyi. Nasi tunaamini ya kwamba labda Mungu atatusaidia, natumaini Yeye atatusaidia.

²²³ Ninaona iko moja kwa moja juu ya mwanamke anayeketi hapa. Ananiangalia, lakini ameketi papa hapa, analia, ameinua mkono wake namna *hii*, hadi usoni mwake, ana kibandiko usoni mwake. Sasa, huenda ikawa ni fimbo iliyompiga, ingeweza kuwa chochote. Unaamini Mungu anaweza kuniambia ni kitu gani kutoka hapa? Ungekubali jambo hilo? Ni kansa. Unaamini ya kwamba Mungu ataiponya? Utalikubali? Vema, bwana, basi unaweza kufanya hivyo. Amina.

²²⁴ Maskini mama huyo aliyeketi hapo, amevaa sweta jeusi, ameushusha mkono wake chini, ameweka kidolechake kinywani mwake, ulikuwa umeinua mkono wako dakika chache zilizopita, kwamba ulikuwa hapa ukitaka maombi. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Unaamini? Basi, kama utaamini kwa moyo wako wote, basi moyo wako hautakusumbua tena, nawe utakuwa mzima. Unaamini kwamba ugonjwa wako wa moyo utakwisha? (Vema, bwana.) wala kamwe huwezi kujua. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuamini, hivyo tu.

²²⁵ Sasa, siwajui watu hao, ni wageni. Sasa, unaniamini mimi? Hii hapa mikono yangu juu, na Biblia yangu hapa, Mimi, nijuavyo mimi, sijawahi kuwaona maishani mwangu, wao ni watu tu wanaoketi hapo.

²²⁶ Hapa. Loo, ni hisia ya jinsi gani! Mungu asifiwe. Ndugu, Roho Mtakatifu! Angalieni, naomba, jaribuni kuona jambo hili. Angalieni papo hapo, kando ya mwanamke huyo, angalieni Nuru hiyo papo hapo. Mnaona kuzunguka-zunguka huko kwa namna hiyo, kwororo, kitu kama mng'aro, kikimshukia moja kwa moja? Hivi hamwezi kuionga? Angalieni, mama huyu tu anayeketi papo hapo.

Anaomba kwa ajili ya mwanaye, anasumbuliwa na akili. Hiyo ni kweli, sivyo, Mama? Inua mkono wako juu kama hiyo ni kweli. Iweni tu na imani.

²²⁷ Hilo lilimgusa mama huyo kando yako, hapo ilitoka moja kwa moja kwa mama huyo hadi kwa mwingine. Je, nyote mna kadi ya maombi? Una kadi ya maombi? La, huna. Vema. Huhitaji moja.

²²⁸ Huyo mama kando yako hapo, ile Nuru iko moja kwa moja juu yake. Angalia tu huku, kwangu, Dada, kwa muda kidogo tu. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Naam. Ni binti yako ndio kwanza afanyiwe upasuaji, unauombea. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Usitie shaka, itakuwa sawa.

Mnaamini?

²²⁹ Unalia nini, Mama? Umechanganyikiwa kabisa, sivyo? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Hatufahamiani. Usilie. Hebu, angalia, Mama...

²³⁰ Usifanye hivyo! Usifanye hivyo! Sitalisema, lakini unajari... unajiandaa, kufanya jambo fulani, wala usilifanye. Halifai kitu! Vema. Achana nalo! Usifanye hivyo! Kaa mbali nalo! Ondoka tu, lipuuze, itakuwa sawa. Kamwe usiutoe uhai, maana haitafaa kitu. Kaa mbali nalo! Unaamini ya kwamba mimi ni mtumishi Wake? Huishi hapa, unaenda Charlotte sasa. Hiyo ni kweli. Bibi Mongolo, wewe rudi, usifanye lolote kulihu, naye Mungu atakuwa pamoja nawe, na kulitatua vizuri.

Mnaamini? Aminini tu, msiwe na shaka. Usitie shaka, amini tu kwa moyo wako wote.

²³¹ Huko nyuma kabisa, huko nyuma kabisa, moja kwa moja huko nyuma, yuko wapi, ambapo mtu huyo amesimama amevaa shati jeupe, mwanamke mwenye ugonjwa wa ngozi, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Mama? Unaukubali, unauamini? Hiyo ni kweli. Mbona, huyo hapo. Simama tu kwa miguu yako, ili uweze tu kumsifu Mungu kwa ajili yake, nao huo utakuacha. Una kadi ya maombi? Huhitaji moja. Unapokuwa na imani kama

hiyo, huhitaji kadi ya maombi. Huo utakuacha, maana kivuli, kilichokuwa kimesimama hapo juu yako, kimeondoka. Unaona?

²³² Huyu hapa mama mmoja ameketi moja kwa moja chini hivi. Yeye ni . . . Mungu, jalia asiukose. Amekuwa na shida, amekuwa na ajali, na yeye, inamfanya ashikwe na vipindi vya udhaifu, kwa namna fulani kama kuzimia. Yeye hatoki hapa, kutoka Georgia. Amini tu, Bibi Griffin, nawe utapona . . . ? . . .

Hanifahamu, simjui mimi. Simama, Mama, mtambue Bwana Yesu kama Mponyaji wako. Mnaamini, marafiki zangu?

²³³ Mama aliyeketi papa hapa nyuma, akiomba. Anamwombea rafiki ambaye ni mlevi sugu, mwininge aliye na uvimbe kwenye ubongo. Aisee, ulikuwa katika mmoja wa mikutano yangu wakati mmoja, uliponywa kansa. Hiyo ni kweli. Unaishi Charleston. Binti Muller, nenda nyumbani sasa, Yesu Kristo anakupa shauku yako. Amina.

²³⁴ Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, ninaamini Roho Mtakatifu amepitia jengo lote. Je, ninyi ni waaminio? Ni wangapi hapa ndani wanaoamini ya kwamba aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa? Mnaamini? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye alisema hivi: "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya"? Mnaamini hilo? Nanyi mlisema ninyi ni waaminio. Sasa, hebu na tuwekeane mikono.

²³⁵ Baba yetu wa Mbinguni, tunalileta kusanyiko hili Kwako, tumekuwa tukizungumza juu ya karama kuu kote katika nyakati, na sisi hapa, tumefungwa moyoni na Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu yuko hapa pamoja nasi, akijidhihirisha Mwenyewe, ikionyesha ya kwamba—ya kwamba Kanisa linapokea ishara Yake ya mwisho kabla tu ya Mungu kugeuka na kulipeleka Kanisa Utukufuni.

²³⁶ Sasa, hebu waaminio hawa . . . Jalia Roho Mtakatifu aangalie chini kwenye miyo ya hao waaminio ambao wameweka mikono yao juu ya mtu mwininge, wakiwaombea, Wewe ulisema, "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa yule, Mungu atamwinua." Ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Nasi tumefundishwa katika miaka yote kwamba popote wawili wanapokusanyika pamoja, ama watatu, utakuwa katikati yao. Nawe huyu hapa usiku wa leo, Bwana, halisi tu kama ulivyokuwa wakati ulipokuja pamoja na Kleopa na hao wengine na kumega mkate, nao wakakutambua Wewe kwa ishara uliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, walijua ulikuwa umefufuka katika wafu, nao wakaenda makwao wenye furaha, wakishangilia, na kusema, "Hakika Bwana amefufuka."

²³⁷ Sasa, Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utaenda pamoja nasi, Bwana. Jalia nguvu za Roho Mtakatifu zimweke huru kila mtu aliye hapa usiku wa leo, ambaye amefungwa na mateso yoyote, ninaposhikana mikono na kundi hili la

wahudumu hapa, kama mtumishi Wako, nikiamini kwa ajili ya kusanyiko hili, nasi tuko katika nia moja, mahali pamoja, naye Roho Mtakatifu yupo hapa kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Ee Mungu, jalia nguvu za ibilisi zivunjwe, na Roho Mtakatifu ashuke juu ya kusanyiko hili la...?...na kutupilia mbali roho mchafu wa kutokuamini, katika Jina la Yesu Kristo.

²³⁸ Ninamwamini Yeye. Ninaamini kila mmoja wenu ameponywa kama tu mtalikubali. Sisi wahudumu, hapa jukwaani, tutaunganisha mikono pamoja kwa umoja wa maombi. Tunaamini kwa moyo wetu wote kwamba Kristo ndiye anayejidhihirisha Mwenyewe hapa mbele zetu. Ni kitu gani? Ni Urimu na Thumimu ikidhihirishwa kwa Neno, Roho Mtakatifu katika ishara ya siku ya mwisho, kabla dunia haijateketezwa.

²³⁹ Loo, jifiche katika Kristo usiku wa leo, kama vile Yeye alivyoahidi, na uwe mzima, kila mmoja wenu. Wote watakaoliamini, tusimame kwa miguu yetu sasa, tunapomwinulia mikono yetu kwa moyo mmoja. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa hatia yangu yote,
Ee nijalie tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

²⁴⁰ Katika Jina la Bwana Yesu...?... 

62-0612 Tazama, Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa
Central Assembly Of God
Columbia, South Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org